SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Wawili** wa familia moja walivyopoteza maisha kwenye ajali barabarani

UKURASA 2



**Suarez afunguka sakata kumzomea Koeman Barca**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatatu Oktoba 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580723

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Elimu, chanjo corona makanisani, misikitini

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**MABALOZI WANAOKWENDA NJE WAPEWA MAELEKEZO**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema mabalozi wanaoteuliwa...

UKURASA WA 4
**MNYIKA AFUNGUKA MRADI WA MAJI**
JOHN Mnyika ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Ubungo na Kibamba...

UKURASA WA 8
**MACHINGA DAR WANENA SABABU KUTOONDOKA**
LICHA ya hatua ya serikali mkoani Dar es Salaam kuwapanga...


## Utafiti wabaini ugonjwa mpya tishio Tanzania

UKURASA 2



Mkazi wa Msumi 'A' Jimbo la Kibamba mkoani Dar es Salaam, Beatrice John, akimkabidhi kidumu chenye maji yasiyo salama wanayotumia, wakazi wa eneo hilo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, wakati wa utiaji saini mkataba kuanza utekelezaji wa Mradi wa Maji Mshikamano-Makabe, jana. **Habari Uk. 4. NA MPIGAPICHA WETU**



## TRA yakusanya tril. 5/- miezi mitatu

UKURASA 3

MICHEZO **SAKHO, KENNEDY WAKO FITI - SIMBA** UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wawili familia moja walivyokufa ajalini

**Na Richard Makore,** MWANZA

BASI linalomilikiwa na kampuni ya Zakaria limegongana na gari dogo aina ya Prado katika kijiji cha Gamasara nje kidogo ya mji wa Tarime, mkoani Mara na kusababisha vifo vya watu wawili.

Kwa mujibu wa mashuhuda, ajali hiyo ilitokea jana asubuhi wakati basi hilo lenye namba za usajili T 906 DLJ likitokea Mwanza na Prado lenye namba T 184 AQT likitokea mjini Tarime.

Ilielezwa kwamba marehemu wote wawili ni ndugu kutoka familia moja na miili yao ilipelekwa kuhifadhiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Abiria wengine katika basi hilo waliopata majeraha walikimbizwa hospitali kwa ajili ya kupatiwa matibu mjini Tarime.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime na Rorya, William Mkonda,

alisema ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu wawili na majeruhi watatu.

Mkonda alisema magari hayo yaligongana uso kwa uso na kuwataka madereva kuwa makini wanapokuwa barabara ili kuepusha vifo kwa watu wasiokuwa na hatia yoyote.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akiongea na wafanyakazi wa benki hiyo katika mdahalo maalum wa kuhamasisha jamii kujikinga na visababishi, uliofanyika ukumbi wa mikutano katika Makao Makuu mapya ya Benki ya CRDB yaliyopo Palm Beach. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Mawasiliano, Tully Esther Mwambapa, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Siaophoro Kishimbo, Daktari Bingwa wa Saratani wa Hospitali ya Kansa ya Ocean Road, pia Rais wa Chama cha Madaktari wa Saratani Tanzania, Dk. Jerry Ndumbalo na Maneja Uendeshaji Hazina Benki ya CRDB, Rose Moleli ambaye ni shuhuda wa gonjwa la kansa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Elimu, chanjo corona kanisani, misikitini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu ya umuhimu wa kuchanja chanjo ya UVIKO-19 kwa waumini kanisani na misikini baada ya ibada.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jijini Dodoma alipokuwa akitoa elimu ya umuhimu wa kuchanja chanjo hiyo kwa watumishi wa Wizara ya Madini.

Prof. Makubi alisema kutokana na utoaji wa elimu ambao unafanywa hivi sasa na wizara yake mwitikio wa watu kuchanja umeongezeka kwa kasi.

"Awali Rais Samia alipozindua chanjo hii, idadi ya watu ilikuwa kwa siku watu wanaochanja ni 20,000, lakini baada ya maneno yale yaliyotokea kwenye mitandao ulishuka hadi kufikia watu 1,000 kwa siku. Lakini hivi sasa baada ya kuanzia kampeni hii ya elimu, idadi imepanda hadi watu 30,000 kuchanja kwa siku," alisema Prof. Makubi.

Alisema hivi sasa wizara yake imezungumza na viongozi wa dini wa makanisa na misikiti mbalimbali nchini ili kuanza kutoa elimu kwa waumini wao kila baada ya ibada kuisha na kutoa chanjo katika eneo husika.

Pia alisema lengo la elimu hiyo ni kuhakikisha kuwa idadi ya watu wanaochanja kwa hiari chanjo ya UVIKO-19 inaongezeka zaidi ya sasa. Aliwataka Watanzania kuwapuuza watu ambao wamekuwa wakitoa kejeli kuhusu chanjo na kupotosha umma.

"Ndugu zangu, chanjo hizi ni salama kabisa tumefanyia vipimo mbalimbali katika mamlaka zetu na kujiridhisha kuwa ni salama, hivyo msidanganyike na watu hata Hayati Rais Magufuli hakuwahi kusema watu wasichanje, lakini alisema kuwa kama zitakuja inabidi tujiridhishe na ndicho wizara tulisisitiza na kimefanyika," alisema Prof. Makubi.

Vilevile, alisema chanjo hiyo inayotolewa nchini ni salama na inafaa kwa watu wote wakiwamo wenye magonjwa ya kisukari, kansa, figo, shinikizo la damu na hata mama mjamzito ni ruksa kuchanja. "Kuna watu wanapotosha kuwa eti mwanamke akichanja anaweza asipate ujauzito kabisa, jambo hili siyo kweli kabisa hakuna mahusiano kati ya chanjo hii na mtu kutopata ujauzito," alisema Prof. Makubi.

Kadhalika, alitoa wito kwa wananchi kuchangamkia chanjo hiyo ambayo inaelekea kuisha kabla ya kuingizwa nyingine.

"Ndugu zangu tuchangamkie chanjo hii ambayo hivi sasa mtu anachanja mara moja tuu, hiyo nyingine ikija mtu atalazimika kuchanja mara mbili," alifafanua.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, alishukuru Wizara ya Afya kwa kutoa elimu kwa watumishi wake ili kuhamasika kuchanja chanjo hiyo na kujikinga na UVIKO-19.

"Pamoja na elimu hii, lakini hapa tulipo yapo maeneo maalum kwa ajili ya kutoa chanjo... mimi nilishachanja, hivyo inawashauri watumishi pia tutumie fursa hii kuchanja na kuacha kusikiliza maneno ya watu wasiyokuwa na weledi wa masuala ya afya," alisema Prof. Msanjila.

# Utafiti wabaini ugonjwa mpya tishio Tanzania

**Na Sanula Athanas**

WATAALAMU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameshauri serikali na wadau kuchukua hatua za haraka kukabiliana na ugonjwa wa homa ya lesptospirosis, ambao wamebaini haufahamiki kwa wengi, lakini unasambaa na kuathiri binadamu na wanyama nchini.

Walitoa rai hiyo wiki iliyopita mkoani Dar es Salaam walipowasilisha ripoti ya utafiti wao uliofanyika kwa miaka 25 kuanzia mwaka 1996 kwa ufadhili wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Katika wasilisho lao hilo, wataalamu hao wa SUA walibainisha kuwa ufahamu wa ugonjwa huo ni mdogo kwa umma na miongoni mwa watoa huduma za fya.

"Kuwapo ongezeko la leptospirosis kwa binadamu kumeripotiwa kwa idadi kubwa katika mikoa mingi ikiwamo Morogoro, Kilimanjaro na Katavi," alisema Dk. Abdul Katakweba wa SUA, ambaye alikuwa sehemu ya utafiti huo.

Alisema ugonjwa huo unaosababishwa na bakteria anayeitwa Leptospira, unaenezwa na panya kwa binadamu na wanyama.

Dk. Katakweba aliongeza kuwa leptospirosis pia huambukizwa kupitia udongo wenye unyevunyevu (tope) na maji, ambamo bakteria huyo anaweza kukaa kwa muda mrefu.

Kulingana na ripoti hiyo, kuna hatari kubwa ya maambikizi ya kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu nchini ikizingatiwa asilimia 70 ya raia wanajihusisha na shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mbali na binadamu, wanyama waliotajwa na wataalamu hao kubainika kuwa na ugonjwa huo ni pamoja na mifugo, ikiwamo ng'ombe, nguruwe, mbuzi, mbwa, kondoo na paka.

"Bakteria husambazwa kwa binadamu na panya na mamalia wengine wadogo kwa kugusa mkojo wao wenye vimelea, nyama na vingine vyenye majimaji," inasomeka sehemu ya ripoti hiyo ya utafiti.

Utafiti unaonyesha kulikuwa na kiwango kikubwa cha leptospirosis mkoani Morogoro (asilimia 10.8-13) mwaka 2015 na Kilimanjaro (asilimia 9-20) mwaka 2013.

Watafiti hao wanasema licha ya ukweli kwamba ugonjwa huo unaweza kutibiwa kwa dawa, ukosefu wa miongozo na usimamizi wake nchini, unaweka watu wengi katika hatari ya kuugua na hata vifo.

Wataalamu hao wa SUA walisema dalili za leptospirosis ni sawa na za magonjwa mengi ya homa, hivyo ni muhimu kuwa na miongozo inayofaa kwa watoa huduma za afya juu ya usimamizi wake, ili kuzuia vifo na kuokoa rasilimali zinazotumika isivyofaa kutibu mardhi mengine ilhali kumbe mgonjwa ana leptospirosis.

"Ni wakati mwafaka watoa huduma za afya wawe na uelewa wa uwapo wa leptospirosis na vituo vya afya viwe na vifaa vinavyohitajika kutambua na kutibu ugonjwa huu," wataalamu hao wanapendekeza katika ripoti yao hiyo ya utafiti.

Kulingana na utafiti huo, kinachofanyika sasa, magonjwa mengi ya homa yanahusishwa na malaria, kasumba iliyojengwa kwa umma na hata miongoni mwa watoa huduma za afya.

"Hii inawafanya watu wengi kuwa kwenye hatari ya kupoteza maisha kutokana na kupewa matibabu ya malaria ilhali wanachougua siyo malaria," wataalamu hao wahadharisha katika ripoti yao hiyo.

Wataalamu hao wa SUA wanashauri miongozo ya udhibiti na matibabu ya magonjwa ya homa izingatie uwezekano wa kuwapo kwa magonjwa mengine yanayofanana na hayo ya homa, ikiwamo leptospirosis.•

HABARI KITAIFA

# TRA yakusanya tril.5/- miezi mitatu

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imekusanya Sh. trilioni 5.151 katika kipindi cha robo mwaka 2021/22, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 17.4 ya lengo lililowekwa la kukusanya Sh. trilioni 5.462.

Makusanyo hayo yameongeza ufanisi wa ukusanyaji mapato kwa asilimia 97.4 ikilinganishwa na yaliyokusanywa kipindi kama hicho kuanzia Julai hadi Septemba 2020/21 zikikusanywa Sh. trilioni 4.4.

Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, aliyasema hayo jana kwenye taarifa yake kuhusu makusanyo ya kodi kwa kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema Julai mwaka jana zilikusanywa Sh. tril. 1.284, huku mwaka huu kipindi kama hicho zikikusanywa Sh. tril 1.535 sawa ukuaji wa asilimia 19.5.

Pia kipindi cha Agosti mwaka jana zilikusanywa Sh. tril. 1.399 na mwaka huu kipindi kama hicho zimekusanywa Sh. tril. 1.645 ambayo ni ukuaji wa asilimia 17.6.

Kidata alisema katika kipindi cha Septemba mwaka jana makusanyo yalikuwa Sh. tril. 1.703 na mwaka huu kipindi kama hicho zimekusanywa Sh. tril. 1.970 ikiwa ni ukuaji wa asilimia 15.

**SABABU ONGEZEKO**

Kidata alisema sababu ya ufanisi wa TRA katika makusanyo ni ulipaji kodi kwa hiari kutoka kwa walipakodi kwenye maeneo ya uchimbaji, mawasiliano na uchukuzi.

Sababu nyingine aliitaja ni kuongezeka kwa uwezo wa walipakodi katika kulipa malimbikizo kunatokana na serikali kuongeza kasi ya kulipa marejesho ya kodi.

Nyingine ni kuimarika uhusiano kati ya TRA na walipakodi, utatuzi wa kodi nje ya mahakama na kutatua malalamiko.

Kidata alitaja sababu nyingine ni kuimarika biashara za kimataifa, kudhibiti Covid-19, kujenga imani kwa wafanyabiashara, mazingira bora ya biashara na miradi ya SGR na wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere.

Alitoa wito kwa wananchi kuungana na serikali katika kukuza maendeleo kwa kuendeleza utamaduni wa kulipa kodi kielektroniki kwa mashine za EFDs pamoja na kutoa risiti kwa wanunuzi bidhaa.

## Majaliwa awapa maelekezo mabalozi wanaokwenda nje

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema mabalozi wanaoteuliwa kuiwakilisha Tanzania nje ya nchi wanapaswa kutanguliza maslahi ya Taifa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Amesema mabalozi hao wanapaswa kutekeleza falsafa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuona kazi zilizoratibiwa zinaendelea kutekelezwa kwa uadilifu mkubwa na uaminifu, ili ziweze kutoa matokeo chanya katika kila kazi zinazofanyika.

Waziri Mkuu alitoa wito huo jana ofisini kwake Mlimwa jijini Dodoma alipokutana na mabalozi saba watakaoiwakilisha Tanzania katika nchi za Uturuki, Sweden, Rwanda, India, Ethiopia, Uswisi na Jamhuri ya Korea.

Mabalozi hao na nchi zao kwenye mabano ni Luteni Jenerali Yacoub Mohamed (Uturuki), Grace Olotu (Sweden), Meja Jenerali Richard Makanzo (Rwanda), Anisa Mbega (India), Innocent Shiyo (Ethiopia), Hoyce Temu (Uswisi) na Togolani Mavura (Jamhuri ya Korea).

Waziri Mkuu alisema mabalozi hao wana jukumu la kukuza uchumi wa Tanzania kupitia diplomasia ya uchumi. "Waheshimiwa mabalozi mna jukumu kubwa la kukuza uchumi wetu. Nendeni mkaimarishe biashara na nchi yetu. Mwangalie sisi tumefanya nini na tumepungua wapi na je, tunaweza kurekebisha vipi?" amesema.

Alisema ili Tanzania iweze kupaa zaidi kiuchumi, inapaswa kukuza sekta ya viwanda hatua ambayo itafanya bidhaa zinazouzwa ziwe ni zile zilizosindikwa. "Mnalo jukumu la kuangalia ni namna gani tunaweza kuongeza uzalishaji na siyo wa mazao ghafi bali yaliyosindikwa. Tunataka tuuze kahawa iliyosindikwa hadi mwisho, na kama ni korosho, tuuze zilizobanguliwa."

"Tanzania tunataka tuimarishe uchumi wetu wa viwanda. Kuna watu wanadai kuwa viwanda vingi vilivyokuwapo zamani vimekufa, lakini wanasahau kwamba teknolojia imebadilika sana. Kwa hiyo leteni watu kwenye uwekezaji wa viwanda, cha msingi wawe ni wale ambao wana historia nzuri kwenye nchi zao (genuine investors)," alisisitiza.

Alisema Tanzania imedhamiria kufufua mazao ya mkonge, michikichi na mbegu za mafuta na akawataka watafute wawekezaji makini ambao watakuja kuwekeza kwenye mazao hayo.

"Sambamba na hilo, muangalie uwezekano wa kupata masoko ya mazao yanayozalishwa nchini. Mnapaswa muwe ni kiungo baina ya nchi yetu na hizo nchi mnazoenda kutuwakilisha.

Muangalie sisi tuna mazao au bidhaa gani na wao wanaweza kuagiza kiasi gani kutoka hapa nchini."

Aliwataka waangalie ni jinsi gani wanaweza kuinua sekta nyingine kama vile utalii kwa kuitangaza Tanzania huko waendako ili kuvutia watalii wengi zaidi.

"Tanzania tuna fukwe nzuri sana kule Zanzibar na kuanzia Tanga hadi Mtwara. "Himizeni wawekezaji wa kujenga hoteli kwenye hizi fukwe ili watalii wakija wakute zile wanazozihitaji."


TAARIFA KWA UMMA

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

MSAMAHA KWA WAAJIRI WENYE MALIMBIKIZO YA MICHANGO NA TOZO ITOKANAYO NA UCHELEWESHAJI WA MICHANGO.

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unapenda kuwataarifu Waajiri wote na Umma kwa ujumla kwamba utatoa msamaha kwa Waajiri wote wenye malimbikizo ya michango na tozo itokanayo na ucheleweshaji wa michango kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

1) Waajiri wote watakaolipa malimbikizo ya michango ifikapo tarehe 30 Novemba, 2021 watapata msamaha wa tozo itokanayo na ucheleweshaji wa michango husika kwa kiwango cha asilimia mia moja (100%).

2) Waajiri wote watakaolipa malimbikizo ya michango ifikapo tarehe 31 Desemba, 2021 watapata msamaha wa tozo itokanayo na ucheleweshaji wa michango husika kwa kiwango cha asilimia sabini na tano (75%).

3) Waajiri wote watakaolipa malimbikizo ya michango ifikapo tarehe 31 Januari, 2022 watapata msamaha wa tozo itokanayo na ucheleweshaji wa michango husika kwa kiwango cha asilimia hamsini (50%).

**Msamaha huu utaanza rasmi tarehe 1 Oktoba, 2021 na unahusu Waajiri wote wenye malimbikizo ya michango na tozo kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2021.**

Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kupitia simu ya bure 0800116773 au tembelea ofisi ya NSSF iliyo karibu nawe.

**Imetolewa na Idara ya Uhusiano na Elimu kwa Umma**

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

NSSF

www.nssf.or.tz

@NssfTanzania

HABARI KITAIFA

# Mkazi Kibamba amkabidhi Waziri wa Maji kidumu cha maji machafu

**Na Frank Monyo**

MKAZI wa Msumi A wilayani Ubungo mkoani Dar es Salaam, Beatrice John, amelazimika kufika katika mkutano akiwa na kidumu cha lita tano chenye maji machafu, kumkabidhi Waziri wa Maji, Juma Aweso.

Alimkabidhi Waziri Aweso jana wakati wa tukio la utiaji saini mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa Maji Mshikamano-Kibamba utakaotekelezwa na Mkandarasi Advent Construction Company, wenye gharama ya Sh. bilioni 5.4 kwa muda wa mwaka mmoja.

Lengo la kufanya hivyo ni kufikisha kilio cha eneo analotoka kwa Waziri Aweso, kuhusu kadhia wanayopata ya kutumia maji machafu kwa miaka 16.

Beatrice alifika kwenye tukio hilo akiwa na dumu la maji machafu la lita tano kisha alipaza sauti katikati ya mkutano huo kwa kusema, "Haya ndio maji tunayotumia, angalieni maji tunayotumia...tunaomba msaada, tunateseka kwa kutumia maji machafu."

Hali hiyo ilimlazimu Waziri Aweso kumuita na kuomba kukabidhiwa maji hayo.

Akizungumza na Nipashe baada ya kuwasilisha maji hayo, alisema wakazi wa eneo lake wamekuwa wakitumia shabu kuweka kwenye maji wanayochota kwenye makorongo waliyochimba, kuyasafisha kwa ajili ya matumizi ya kila siku.

Aidha, alisema wamekuwa wakibabuka ngozi baada ya matumizi ya maji hayo na kuwafanya ngozi zao kufanana mithili ya kenge.

"Tangu nimeamia huku mwaka 2005 sisi ni wa kuteseka tu, tumekuwa tukiamka saa 10 alfajiri kwenda kuchimba makorongo kwa ajili ya kupata maji, baada ya kuchimba mpaka saa saba mchana ndiyo tunapata maji, tunateseka sana," alisimulia mama huyo.

Alisema katika familia yake kwa siku anatumia ndoo zaidi ya 10 za maji, huku akibainisha kuwa kutokana na kutokuwa na uwezo wa kununua maji kwenye magari, hulazimika kulala bila kuoga yeye na familia yake.

"Huku kuna magari yanauza maji, ndoo moja wanauza Sh. 500, siku nikipata mia 500 nanunua maji kwa ajili ya kunywa, lakini siku nikikosa ndio tunatumia shabu kusafisha maji ambayo tunachota kwenye makorogo," alisema Beatice.

Akielezea mamna wanavyotumia shabu kusafisha maji, alisema: "Baada ya kuchota maji machafu, tunachukua shabu na kuweka kwenye maji tunasubiri baada ya muda maji machafu yanashuka chini, masafi yanapanda juu... kwa ndoo 12 huwa tunatumia shabu kikombe kimoja ambayo tunanunua ya kupima kwa gharama ya Sh. 500 ambayo tunaweza kuitumia hadi mwezi mmoja".

**KUHUSU MRADI**

Mradi huo utanufaisha maeneo ya Mshikamano, Mpiji, Magohe, Msakuzi Kusini, Msakuzi Kaskazini, Machimbo, Majengo mapya, Dodoma, Luguruni Lapaz, Mbezi Inn, Magari Saba, Magayana na Njia Panda Makondeni.

Maeneo mengine yatakayonufaika na mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ni TAKUKRU, Kwa Gamba, Luguruni Dampo, Luguruni KKKT, Rising Star, Msakuzi Supermarket, Amani Street, Miti mirefu, Madafu, Kwa Mfala, Chikongowe, Masaki Street, Mbezi Msumi, Machimbo na Mageti.

Akizungumza katika tukio hilo, Waziri Aweso alisema baada ya Rais Samia kumwapishwa alimuita na kumweleza kuwa katika maeneo yote aliyopita wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu kilio kikubwa cha wananchi kilikuwa ni maji na asilimia kubwa wanaoteseka ni kinamama.

Aidha, aliagiza wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi huo kulipwa fidia zao haraka, huku akimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Maji, kumlipa mkandarasi malipo ya awali ndani ya wiki moja ili aanze kazi haraka.

"Luhemeja (Ofisa Mtendaji Mkuu DASAWA) ujipange pamoja na makandarasi, mimi ni kijana bwana ukizingua tunazinguana, wakati mwingine tunachelewa kuhudumia wananchi kwa kuonekana haya, ndugu zangu mimi sitamuonea haya mtu," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema kuwa utekelezaji wa mradi huo unahusisha ulazaji wa bomba la chuma lenye ukubwa wa kipenyo cha inchi 16 linalosafirisha maji kutoka mtambo wa Ruvu Juu hadi kwenye kituo cha kusukuma maji eneo la Mbezi Inn.

Alisema mradi huyo pia utakuwa na uwezo wa kusafirisha maji lita milioni 23,300 kwa siku ambazo zitatosheleza mahitaji ya wananchi 179,476.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Kamati Kuu Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM iliyokutana Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Mnyika afunguka mradi wa maji

**Na Christina Mwakangale**

JOHN Mnyika ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Ubungo na Kibamba, mkoani Dar es Salaam, amesema matunda ya mradi wa maji kwa wakazi wa Kibamba yametokana na juhudi zake tangu akiiongoza Ubungo, kabla haijagawanywa.

Amesema ukweli ni kwamba upatikanaji wa maji katika Jimbo la Kibamba ni wa asilimia kubwa ikilinganishwa na mengine ikiwamo Kigamboni hata Ukonga.

Mnyika ambaye sasa ni Katibu Mkuu Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), aliyasema hayo jana akizungumza na Nipashe akielezea kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji wilayani Ubungo uliozinduliwa jana mkoani Dar es Salaam na kutiwa saini na Waziri wa Maji Jumaa Awesso.

"Ni vyema Wizara ya Maji na DAWASA wakasema ukweli juu ya kazi kubwa iliyofanyika kwa miaka 10 kati ya 2010 na 2020, ambayo ndio imefanya upatikanaji wa maji kwa majimbo ya Ubungo na Kibamba kwa pamoja, kufikia wastani unaozidi asilimia 90.

"Wakati naingia kuwa mbunge wa Ubungo mwaka 2010, ikiwa na majimbo ya Ubungo na Kibamba upatikanaji wa maji ulikuwa chini ya asilimia 50. Ikumbukwe kwamba wabunge wa CCM na TANU (ukiondoa kipindi kifupi cha Lamwai wa NCCR) ndio waliokuwa wakiongoza maeneo hayo," alisema Mnyika.

Mnyika alibainisha kwamba kwa miaka 10 ya kipindi alichokuwa mbunge, upatikanaji wa maji ni msukumo wa kipindi chake, kuleta maji katika jimbo la Ubungo na baadaye Jimbo la Kibamba kutokana na hoja zake, akiwa bungeni.

"Kupitia michango, hoja binafsi, maswali na njia nyingine za kibunge na nje ya bunge, kupitia ziara za jimboni, vikao na DAWASCO na DAWASA, maandamano ya wananchi kuhusu maji na mawasiliano ya mara kwa mara ya moja kwa moja kati ya mbunge na mamlaka zinazohusika, ndio hiki leo.

"Rais Kikwete alitembelea jimboni Ubungo mwaka 2013 na Rais Magufuli (hayati) wakati akizindua ujenzi wa barabara jimboni Kibamba mwaka 2018. Hivyo hivyo kwa mawaziri na manaibu waziri wa maji waliopita katika kipindi hicho," alieleza Mnyika.

Aidha, alitoa wito kwamba kiasi cha shilling bilioni 5.4 zilizotengwa katika mradi huo, zitoewe kwa wakati ili wananchi wanufaike.

# Watumia machela ya miti kusafirisha wagonjwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI wa Kijiji cha Kitewele wilayani Ludewa mkoani Njombe wanalazimika kusafirisha wagonjwa kwa machela za fimbo za miti na mihanzi umbali wa zaidi ya kilometa 32 kufuata huduma za afya.

Hatua hiyo inatokana na ubovu wa barabara ambayo haipitiki kwa gari inayounganisha vijiji vya Madunda, Kitewele na Makonde iliyochimbwa miaka michache iliyopita kwa mikono na wakazi wa Kijiji cha Kitewele chenye wakazi zaidi ya 1,000 huku lengo kuu likiwa ni kufungua mawasiliano ambayo yaliwafanya kuishi kama watu waliojitenga.

Wakitoa malalamiko yao katika mkutano wa Mbunge wa jimbo hilo, Joseph Kamonga wenye lengo la kusikiliza kero za wananchi, wakazi hao wakiwamo Beno Lwiva na Lasilida Haule, walisema katika kijiji chao kuna zahanati, lakini haifikiki vyombo vya moto na ikitokea mgonjwa analetwa ama kupata rufani hulazimika kutengeneza machela za miti na kutembea umbali mrefu hali ambayo inasababisha baadhi yao kupoteza maisha wakiwa njiani.

"Ndugu zetu wengi wanapoteza maisha kwasababu ya ubovu wa barabara hii, tunabeba kwenye machela za miti ya mihanzi kupeleka wapendwa wetu Hospitali ya Wilaya ya Ludewa na Milo hivyo tunaomba mtusaidie mheshimiwa mbunge wetu," alisema Beno Lwiva.

Akijibu changamoto hiyo Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Ludewa, Enhad Willa, alisema tayari ameitazama barabara hiyo na kuelewa maeneo yote korofi hivyo, ili iweze kukarabatiwa inapaswa kusajiliwa kwenye barabara za wakala huo na mwaka ujao iweze kutengewa bajeti ya kutosha.

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MCFIELD KALUA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 757 DPL – NISSAN X-TRAIL.** CHASSIS NAMBA **NT30159630.** ENGINE NAMBA **QR20599038A.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/KIL/RB/420036/2021.**

116489202

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TAARIFA KWA UMMA

## UNUNUZI, UUZAJI NA USAJILI WA MAGARI BILA KUFUATA TARATIBU NA UHAKIKI KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO

Kwa kuzingatia Kifungu Na. 117, 119 na 200 vya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004, **ikisomwa kwa pamoja na Kifungu Na. 11 cha Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973,** Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuufahamisha na kuukumbusha umma kufuata taratibu zilizoanishwa kwa mujibu wa sheria wakati wa ununuzi, uuzaji na uhamishaji umiliki wa magari kabla ya kupata usajili wa magari hayo. Hapa siku za karibuni tumebaini ukiukwaji wa sheria katika maeneo yafuatayo:-

1. **Magari Yaliyoingizwa Nchini kwa Msamaha wa Kodi**
   Mtu yeyote anayehitaji kuuza, kununua au kubadili umiliki wa gari ambalo lina msamaha wa kodi, anapaswa kufika ofisi ya karibu ya Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya kujua kiasi cha kodi anachopaswa kulipa kabla ya kununua na kubadili umiliki. Kutumia gari hilo bila kufuata utaratibu huu ni kosa kisheria.

2. **Magari Yaliyoingizwa Nchini kwa Hati ya Muda Mfupi (Temporary Import)**
   Magari yote yalioyoingizwa nchini kwa hati ya muda mfupi kwa lengo la utekelezaji wa shughuli maalum iliyoidhinishwa kwa mujibu wa sharia kama iliyotajwa katika Kifungu Na. 136 cha sheria iliyotajwa hapo juu, yakiwemo magari binafsi, yamepewa muda maalum wa ukamilishaji wa shughuli hiyo ya kuwepo kwao hapa nchini. Wananchi wote pamoja na waigizaji wa magari hayo, wanatahadharishwa kuwa muda huo ukiisha yanapaswa kurudishwa nchi yalikotoka. Kuendelea kutumia magari hayo nje ya muda ulioanishwa ni kosa kisheria.

   Aidha, yeyote atakayehitaji kuuza, kununua au kubadili umiliki wa magari hayo ni lazima afike ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya uhakiki na kupewa taratibu za kufuata,

3. **Magari Yaliyoingizwa Nchini Kinyume na Sheria**
   Haya ni magari yaliyoingia nchini bila ya kufuata taratibu, ama kwa njia ya magendo ama Transit. Tunawakumbusha wote wanaoingiza magari nchini kufuata taratibu zilizowekwa ikiwemo kupita katika njia zilizoainishwa.

**Kwa mantiki hiyo:** Wananchi wote wanashauriwa kuwa wanapotaka kununua gari yoyote, kudai nyaraka zilizotumika kuingiza gari hiyo nchini. Aidha wanunuzi hao wanatakiwa kuhakiki nyaraka hizo katika ofisi za TRA zilizo karibu.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi**
**Idara ya Huduma na Elimu kwa Walipakodi**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

116489202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF mulikeni ahadi hizi za wanasiasa zisituharibie ligi

**IKIWA** ndiyo kwanza mwanzo wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2021/22 wakati timu zote 16 shiriki zikiwa zimecheza mechi mbili kwenye mzunguko wa kwanza, ushindani unaonekana kuwa mkubwa pengine kuliko misimu yote iliyopita ndani ya muongo huu.

Kabla ya mechi tatu za jana, Mtibwa Sugar ikiikaribisha Tanzania Prisons, Mbeya City ikiwa mwenyeji wa Mbeya Kwanza FC na Namungo FC ikiwa nyumbani kuialika Kagera Sugar, hakuna timu yoyote ilishinda zaidi ya mabao mawili kwenye mechi hizo za awali, jambo ambalo linaonyesha itakuwa ni ligi ngumu zaidi msimu huu.

Lakini hadi sasa ni timu ya Polisi Tanzania pekee iliyoongoza kwa kushinda mechi zote mbili kwa mabao mawili, ikianza kwa kuichapa KMC FC mabao 2-0 kisha ikapata ushindi wa 2-1 dhidi ya Azam FC. Timu nyingine ni Namungo ambayo iliifunga Geita Gold mabao 2-0 na zingine zote zikipata ushindi wa bao moja, suluhu ama sare 1-1. Ugumu na ushindani huo mkubwa ndio tunaoutaka katika ligi yetu kwani utaongeza mvuto, hivyo kuvutia wawekezaji wengi na hatimaye kuinua vipato vya wachezaji na klabu kwa ujumla, hivyo hauna budi kulindwa na kusimamiwa kwa makini zaidi kutoka kwa wote wenye dhamana na soka letu husuan Shirikisho la Soka Mpira wa Miguu nchini (TFF) kwa kushirikiana na Bodi yake ya Ligi, TPLB.

Hata hivyo, tayari kumeibuka wanasiasa mbalimbali ambao wamekuwa wakiahidi na kutoa motisha kwa baadhi ya klabu za mikoa yao ama wanayoiongoza au walipozaliwa, wakiweka donge nono mezani kama zikishinda kwa baadhi ya timu.

Kwa hakika si jambo baya, lakini kwa namna ahadi hizo zinavyotolewa, kama zikiachwa kuendelea hivyo kuna uwezekano mkubwa tukashuhudia ligi mbaya zaidi ya ukiukwaji wa kanuni kwa kupanga matokeo.

Mechi ya Biashara United dhidi ya Simba katika Uwanja wa Karume mjini Musoma, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi aliahidi timu hiyo ikishinda dhidi ya mabingwa hao watetezi atatoa motisha wa Sh. milioni 15 na endapo itatoka sare ataipa milioni 10, ahadi ambayo aliitekeleza kwa kutoka suluhu katika mchezo huo.

Lakini pia wakati Dodoma Jiji FC ikiikaribisha Simba, Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, aliahidi kuipa donge kama hilo kama itaibuka na ushindi, lakini ikalikosa baada ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao kushinda bao 1-0. Nipashe tunaamini ni ahadi nzuri kwa kuongeza motisha kwa wachezaji, lakini kwa nini iwe zinapocheza na Simba pekee, badala ya kutolewa kwa angalau kila inaposhinda mchezo wake wa nyumbani na ikiwezekana hata ugenini? Tunasema hivyo, hasa kwa kutambua si suala la kufichika kwamba Simba na Yanga zimeigawa nchi katika makundi mawili, hivyo viongozi wa timu hizo upande mmoja unaweza kwa nia ovu kabisa wakatumia mwanya huo wa mashabiki ama wanachama wao viongozi wakisiasa kwa mgongo kwamba ni timu zao, kupenyeza fedha za kupanga matokeo kwa madai ni motisha kutoka kwa viongozi wa mikoa yao.

Hilo ni moja lakini, waamuzi nao hawana budi kufuata kanuni na sheria 17 za soka hususan usalama wa kulinda afya za wachezaji uwanjani kwani kwa namna tulivyoshuhudia rafu mbaya zilizoonyeshwa na timu hizo baada ya kuahidiwa motisha huo, ni wazi kuna dalili msimu huu baadhi wakapata majeraha mabaya yanayoweza kuwasababishia kushindwa kucheza soka kabisa.

Katika hilo tulishuhudia mechi mechi hizo mbili wachezaji watano wa Simba wakishindwa kuendelea na mechi kutokana na kuchezewa rafu mbaya, hivyo ni wakati pia kwa TFF na TPLB kutupia waamuzi jicho mapema ili kuhakikisha wanalinda afya za wachezaji kwa kuchezesha kwa haki.

Kama tunataka tuwe na ligi bora zitakazowavutia mashabiki na wawekezaji pia, ni lazima waamuzi wanapaswa kuacha woga na kutoa kadi iwe ya njano ama nyekundu hata kama ni mwanzo wa mchezo, pale inapostahili kufanya hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Ligi Bora 2021/22 inawezekana, waamuzi mulikeni rafu za kijinga

**INAWEZEKANA** kabisa tukaona msimu bora kabisa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kuliko misimu mingi ya hivi karibuni. Ni kwa jinsi mechi zilivyoanza, timu zilivyopambana kwenye mechi nane za mwanzo tu imeonekana kuwa hakuna kibonde haikuonekana tofauti ya timu iliyokuwa kwenye Ligi Kuu wala iliyopanda.

Kabla ya mechi za jana jioni hakukuwa na timu iliyoshinda zaidi ya mabao mawili. Na timu zilizoshinda mabao hayo zilikuwa ni mbili tu. Polisi Tanzania ndiyo iliyoongoza kwa kushinda mechi zote mbili mabao mawili, iliichapa KMC mabao 2-0, halafu ikatoa kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Azam FC.

Nyingine ni Namungo ambayo iliifunga Geita Gold mabao 2-0, hivyo yoyote aliyedhani kuwa Geita Gold ni kibonde kwa sababu imepanda Ligi Kuu na inacheza kwa mara ya kwanza amekosea. Juzi ilifungwa kwa tabu na Yanga bao 1-0, tena ikiwa ugenini na kwa mara ya kwanza ikikanyaga Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ilicheza kama timu zoefu. Kwa kawaida timu kama Simba au Yanga timu ikiingia kichwa kichwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa, unaweza ukaondoka na kapu la mabao.

Ni kwa sababu ndiyo uwanja ambao Simba na Yanga hazivuni pointi tu, lakini ndiyo sehemu ya kupatia mabao mengi ambayo yanaweza kuamua ubingwa wao mwisho wa msimu. Ndiyo sehemu ambayo salama zaidi kupata ushindi mkubwa kuliko mikoani ambako viwanja vinakuwa si rafiki kwao.

Mbeya Kwanza nayo si timu ya kitoto. Ikaitwanga Mtibwa Sugar bao 1-0 kwenye mechi ya ufunguzi. Timu inayoshiriki michuano ya kimataifa Azam FC, mpaka sasa haijapata ushindi wowote ule, ikiwa imechezea mechi mbili, ikapata sare ya bao 1-1 dhidi ya Coastal Union, na kufungwa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania.

Biashara United ambayo nayo kama Azam inashiriki Kombe la Shirikisho Afrika, ina pointi moja, ikiipata kwa suluhu dhidi ya Simba, lakini ikachapwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Ruvu Shooting.

Kama alivyowahi kusema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo siku moja kabla ya kuanza Ligi Kuu msimu huu alisema anatarajia ligi itakuwa ngumu na bora kuliko msimu uliopita. Na kweli, tumeona hivyo japo kwenye mechi za raundi ya kwanza.

Wadau na wapenzi wa soka wanaomba hali iendelee kuwa hivi ili kuinua soka la Tanzania, na kuwa na Ligi Bora itakayovutia mashabiki wengi wa soka Afrika, ili kupata wadhamini wengi zaidi.

Isiwe tu ni nguvu za soda, baada ya raundi tatu hali inarudi kama kawaida, tuanze kuziona timu zikijitenga, Simba, Yanga na Azam ndiyo zikionekana kuutaka zaidi ubingwa na zingine zikionekana kusindikiza.

Ni kweli bingwa ni lazima awe mmoja, lakini hata timu zilizobaki hata kama zinaonekana ziko mbali nao, lakini zionekane kuzipa changamoto timu zinazotaka kwenda kuutwaa.

Tena kwa sasa timu nne za juu kwenye Ligi ya Tanzania, tatu au zote zinaweza kucheza michuano ya kimataifa, ndiyo tunatarajia ushindani huu uendelee hadi mwisho.

Tatizo nililoliona ni baadhi ya timu, kupania kuwaumiza wachezaji wa timu pinzani. Nimeona baadhi ya mechi kuna wachezaji wanacheza bila kujali afya za wenzao. Nadhani wachezaji wengi wa Kitanzania kutokulia kwenye vituo vya soka kunachangia. Kuna rafu za kutaka kuwaumiza kabisa wachezaji na kuwafanya kuwa walemavu au wasicheze tena soka. Hii ni mbaya sana, yeyote anayeitwa mchezaji si kwa sababu ya kucheza rafu ambazo si za kimpira. Angeenda tu kucheza karate, kung-fu, judo au mieleka. Mchezaji ni yule ambaye anatumia kipaji chake, kuchezea mpira, kumnyang'anya mwenzake kwa ufundi, kuzuia kwa ustadi na kumpita mchezaji mwenzake kwa kipaji alichozaliwa. Nguvu kwenye mpira inatumika, lakini kila mchezaji anajua nguvu inatumika sehemu gani na wakati gani na si kucheza rafu.

Cha ajabu ni kwamba baadhi ya waamuzi wamekuwa wagumu kutoa maamuzi, kana kwamba na wao ni waamuzi wa ngumi, judo au kung-fu.

Kama tunataka tuwe na ligi bora ni lazima waamuzi wasiwe waoga. Waache mpira uchezwe uwanjani na wachezaji wanaotaka kuonyesha vipaji vyao ili kuvutia mashabiki wengi kwenda uwanjani na kuangalia kwenye televisheni. Na hii itasababisha mashabiki wa mpira waongezeke na kupata udhamini mnono pia.

Ni mwamuzi pekee ndiye anayeweza kusababisha soka likachezwa kwa nidhamu, lakini woga, au kuacha kwanza hadi baadaye, ndiyo inasababisha mchezo unakuwa wa fujo na yeye mwenyewe kushindwa kuamua nini afanye kwa sababu ameshaachia sana rafu.

Kwa wenzetu Ulaya au hata Ligi ya Mabingwa Afrika huwezi kuona vitu vya aina ile. Waamuzi hawaruhusu rafu za kijinga kama tulivyoziona kwenye mechi ya Dodoma Jiji dhidi ya Simba. Kule rafu moja tu ya kijinga ni kadi nyekundu. Huku mchezaji mmoja anaweza kufanya tatu, akasababisha wachezaji watatu wakatoka nje, ndiyo akapata kadi ya njano.

Tunaweza kuwa tunataka kuwa na ligi bora, lakini ni lazima baadhi ya waamuzi nao wawe bora. Wasiwe waoga. Wasimamie sheria za soka. Wawe na mamlaka uwanjani na kusimamia soka lichezwe kwa nidhamu. Mwamuzi anayechezesha na kukubali lichezwe kama mechi za mitaani zamani tukiita 'Urlando', 'Bundesliga', au 'Uruguay', yaani kuchezeana rafu, miguu ya shingo, mgongoni, tumboni, viwiko, halafu hachukui hatua, hafai kwenye soka la kisasa.



Mtaalamu wa mifumo ya kompyuta wa Vodacom Tanzania, Omari Amiri, akionyesha jinsi ya kuitumia kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kisarawe, Mwanana Msumi (wapili kushoto), baada ya kampuni hiyo kutoa kompyuta 15, TV, Router na samani kwa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Jokate Mwegelo wilayani Kisarawe, mkoani Pwani jana. Lengo ni kuhakikisha wanafunzi wanapata maudhui ya elimu bure kupitia tovuti ya e-fahamu. Wapili kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Vodacom Tanzania, Jacqueline Materu na kushoto ni Ofisa Elimu Wilaya ya Kisarawe, Alice Nkwera. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machinga wa Dar es Salaam wanena

**Na Maulid Mmbaga**

LICHA ya hatua ya serikali mkoani Dar es Salaam kuwapanga wafanyabiashara ndogodogo na kuwataka waondoke maeneo yasiyo rasmi, baadhi yao wanaonekana kukaidi agizo hilo na kuendelea na shughuli zao kama kawaida.

Baadhi ya wafanyabiashara hao waliofuatwa na Nipashe akiwamo Hadija Ramadhani anayejishughulisha na uuzaji wa chakula na vinywaji eneo la Vingunguti, alidai suala la kuvunjiwa vibanda kwa upande wake anaona ni kutotendewa haki.

Alisema ingawa kuwa wakaidi, lakini wengine wamekubali kuwa hawatajenga vibanda, hawatawasha moto barabarani na kuomba waruhusiwe kupika nyumbani na kuja kuuza maeneo hayo ili wapate ridhiki kwa kuwa maeneo waliyopangiwa alidai hakuna biashara.

"Kwa wale walioambiwa wasitumie moto watajitahidi wapike majumbani na kwamba tusijenge vibanda sawa tumekubali, ila watuachie tuwe tunakuja kuuza hapa ili na sisi tupate ridhiki, huko wanapotaka sisi kwenda kusema kweli biashara hakuna.

"Mwisho wa siku unachoka unarudi kukaa nyumbani na hali ndio inazidi kuwa mbaya zaidi, watoto wanataka kula, wakue, wasome na mambo mengine yaende, hivyo tunaomba watuhurumie tuwe tunaweka meza tukimaliza tunatoa ilimradi kuwe kweupe kama wanavyotaka na vibanda tumeacha hatujengi," alisema Ramadhani.

Fatuma Omary, mfanyabiashara katika eneo hilo alidai kuwa, walitangaziwa kupewa muda wa mwezi mmoja wa kuondoa vibanda vyao na kuondoka katika maeneo ya barabarani kuhamishia biashara katika masoko waliyopangiwa ambayo ni Machinga Complex, Kisutu, Bom'bom na Kijilajila, lakini muda waliopewa haukuisha vibanda vyao vikabomolewa na kuharibiwa bidhaa zao.

Alisema Septemba 23, mwaka huu, walipita watu kuwatangazia kwamba ifikapo Oktoba mosi wabomoe vibanda vyao, lakini kabla siku husika haijafika, Septemba 24 asubuhi wakakuta vibanda vyao vimebomolewa jambo ambalo lilikuwa kinyume na maelekezo ya tangazo, huku akidai kwamba wengine biashara zao ni ndogo hawawezi kumudu sehemu za kulipia.

"Bishara ninayoifanya napika kilo mbili na wakati mwingine unakuta haziishi, sidhani kwamba ninaweza kwenda kukodi fremu, sehemu walizotuambia tuende ni ngumu, kila tukienda tunawaangalia na wenzetu walioko kule hali zao ni ngumu wanalia biashara hakuna wanatuambia bora tulivyokuwapo Kariakoo kuliko huku.

"Wengine tunaona kuanzia asubuhi mpaka mchana vitafunio havijaisha, je, chakula cha mchana itakuwaje? Huku tulipo tuna wateja wetu wengi ambao ni watu wa viwandani, kidogo ukija unauza tunapata ridhiki maisha yanasonga tofauti na kule," alisema Omary.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, alipofuatwa kuzungumzia malalamiko hayo alisema, zipo sheria mbalimbali na miongozo iliyowekwa kwa ajili ya upangiliaji wa jiji na hairuhusu mtu kufanya biashara maeneo ya hifadhi ya barabara, kwenye njia za wapita kwa miguu na kujenga au kuweka meza juu ya mifereji kama mwongozo wa Mkuu wa Mkoa Amos Makalla ulivyo elekeza.

"Wanaoendelea kufanya biashara katika maeneo ambayo tuliwaondoa ni wakaidi, tumewapa muda wa mwezi mmoja wa kujiandaa waondoke kwa hiari yao, hatujaruhusu watu kuendelea kufanya biashara katika maeneo hayo wala kupika, mwongozo wa mkuu wa mkoa ufuatwe, kama mtu anachangamoto ya eneo la kufanyia biashara aje halmashauri tutampatia, soko la Machinga Complex wapo wenzao wanaendelea na biashara bila shida yoyote," alisema Shauri.

Naye mfanyabiashara Alli Shekonga, alidai kwamba suala la vibanda kubomolewa kwa upande wake anaona ni sahihi kwa kuwa limesaidia mazingira hayo kuonekana vizuri, wazi na safi.

"Katika maeneo haya kulikuwa na baadhi ya watu walikuwa wakipika barabarani na kusababisha kero kwa wapiti kwa miguu suala ambalo lilikuwa linanikwaza kwa muda mrefu kwani watu hao walikuwa pia wanasababisha msongamano watu walikuwa wanashindwa kupita kwa urahisi," alisema Shekonga.

Riziki Hemedi ambaye ni mfanyabiashara, alidai kwamba kuna baadhi wameshindwa kutumia vizuri uhuru waliopewa jambo lililosababisha serikali kufikia hatua ya kuwaondoa katika maeneo wanakofanyia biashara.

"Mimi nakaa Chanika nauza vinywaji huku, lakini ukija asubuhi saa 11 unakuta moshi umeshazagaa watu wamesha washa moto barabarani, wakati mwingine wanapita wageni wanatupiga picha kutokana na mazingira yetu yalivyo, hadi wengine tulikuwa tunawafokea na kuwakataza wasitupige picha, siwezi kusema uongo kwasababu eti na mimi ninafanya biashara lazima niseme ukweli.

"Sisi wafanyabiashara tunapewa fursa, lakini tunashindwa kuzitumia, tunazitumia vibaya, tunakosa ustaarabu, tunajua sehemu hii sio rasmi, lakini mwingine anajenga banda na kuweka zege kabisa, wanapika, wanaosha vyombo, wakati mwingine anaona jiko la mkaa halifai anaweka la kuni, na wengine wanafulia nguo hapo hapo maji wanamwaga barabarani kitu ambacho sio sahihi tumepewa uhuru lakini kuutumia tumeshindwa," alisema Riziki.

## Kamati Kuu CCM yawapongeza Samia, Mwinyi

**Na Beatrice Shayo**

KAMATI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kushiriki na kuhutubia Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kuihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa katika uongozi wake Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na mataifa na wadau wengine wa maendeleo duniani kutatua changamoto zinazoukabili ulimwengu kwa sasa.

Taarifa iliyotolewa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ilieleza kuwa Kamati Kuu hiyo ilikutana katika kikao maalum jana Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma, ikiongozwa na Mwenyekiti wake Rais Samia.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Kamati Kuu imeridhishwa na mwenendo wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa jinsi inavyoimarisha diplomasia ya uchumi na sasa wawekezaji mbalimbali wameendelea kuvutiwa na kufanya uwekezaji nchini, jambo ambalo litashamirisha shughuli za maendeleo na kufungua uchumi wa nchi.

Kamati Kuu pia ilimpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuiongoza vyema Zanzibar na kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2020-2025 inaendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa.

Kadhalika, ilieleza kuwa imepokea taarifa ya ziara ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa iliyoongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo iliyofanyika kuanzia Septemba 15 hadi 21 , mwaka huu katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Njombe, kwamba serikali imeahidi kufanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na chama katika ziara hiyo.

HABARI KITAIFA

# Meya Dar aonyesha fursa ya utalii

**Na Sabato Kasika**

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, amesema ufukwe ulipo kando ya Barabara ya Barrack Obama Dar es Salaam uliopewa jina la 'Ilala Carnival', utakuwa kivutio cha utalii kwa wazawa na wageni.

Alisema hayo juzi katika tamasha la uzinduzi wa ufukwe huo umekuwa ukijulikana kama 'Beach ya Dengu', na kufafanua kuwa hiyo ni fursa kwa watu kufanya ziara ya kujua historia na vivutio vya Jiji la Dar es Salaam.

"Kwa kutumia basi letu la utalii wananchi wamezunguka katika vivutio vya jiji bila kulipa chochote, na uzinduzi huu hautakuwa wa mwisho bali utakuwa ukifanyika kila baada ya miezi mitatu kuhamasisha watu kuja kupumzika," alisema Kumbilamoto. Aidha, Meya huyo alisema, jiji halina mpango wa kuufanya ufukwe kuwa chanzo chake cha mapato, badala yake watu watakuwa wanakwenda kupunga hewa na kupumzika bure.

"Vilevile tuna mpango wa kujenga kituo cha polisi na kutakuwa na doria inayofanyika mara kwa mara, lakini pia kwenye suala la usafi, vitajengwa vyoo vya kisasa ili watalii na wenyeji watakaofika waweze kuvitumia," alisema.

Mbunge wa Ilala Mussa, Azzan Zungu, alisema ufukwe huo utasaidia kutangaza utalii wa ndani ya jiji, na pia watu wataondoka na mtindo wa kupumzika baa na badala yake watakwenda katika eneo hilo na familia zao.

"Lakini pia ninaamini kwamba, wafanyabiashara wadogo watatumia ufukwe huu kufanya shughuli zao na kujiingizia kipato ambao kitasaidia kuinua uchumi wao," alisema Zungu.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngwilabuzu Ludigija, alisema, tamasha hilo litakuwa endelevu kwa kufanyika kila baada ya miezi mitatu na kwamba kutakuwa na viabanda vya biashara ambavyo havitakuwa vya kudumu.

"Ilala tunajipanga kujijenga kiuchumi kwa njia ya kijitangaza kitalii zaidi pia wakazi wake wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii, hivyo hapa patakuwa ni sehemu ya kijipatia mapumziko ambapo kwa baadaye watawekeza michezo ya watoto ili iwe nafuu watu kutembea na familia zao," alisema Ludigija.

Mkuu wa Maudhui wa Clouds Media Group (CMG), Sebastian Maganga, ambao ni waandaji wa tamasha hilo, alishukuru Jiji la Dar es Salaam, kuwatunuku uratibu wa 'Ilala Carnival'.




Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Exim Tanzania wakiongozwa na Meneja Mkuu wa Kitengo cha Mikopo wa benki hiyo, Gesela Swai (kulia), wakikabidhi msaada wa mahitaji muhimu ikiwamo magodoro, mashuka, sabuni na vyakula kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Watoto Wetu Tanzania, kilichoko Goba, jijini Dar es Salaam, Evans Tegete, wafanyakazi hao walipotembelea kituo hicho mwishoni mwa wiki ili kufurahia pamoja na watoto hao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SGA yamridhisha RPC polisi jamii

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi nchini ya SGA imepongezwa kwa juhudi zake ambazo zimekuwa za msaada mkubwa kwa Jeshi la Polisi nchini katika kutekeleza majukumu yake.

Pongezi hizo zimetolewa na Kamanda wa Polisi Wilaya ya Kinondoni, SSP Ally Kwendo, wakati wa uzinduzi wa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na kampuni ya SGA.

Alisema SGA imekuwa inaendelea kutoa ushirikiano wake huo maeneo yote nchini kupitia dhana ya ulinzi shirikishi kupitia polisi jamii, ambapo alitoa wito kwa kampuni nyingine za binafsi za ulinzi kuiga kazi nzuri unazofanywa na kampuni ya SGA. Polisi jamii ni dhana ya kushirikisha jamii kwa lengo la kuhakikisha amani na usalama unakuweko katika maeneo yote nchini.

"SGA imekuwa washirika wakubwa wa Jeshi la Polisi Tanzania hata kabla ya wazo la polisi jamii halijaanzishwa hapa nchini na wamekuwa wakitoa ushirikiano wao nchini kote", alisema SSP Wendo.

Aliongeza kuwa makampuni ya ulinzi ya kibinafsi yako mbele katika kutekeleza majukumu ambapo alisema wafanyakazi wa makampuni hayo wako mstari wa mbele kila mara katika kuzuia uhalifu huku wakihakikisha usalama unakuwekmo maeneo wanayotoa huduma zao.

"Jeshi la Polisi tunakusudia kuwajengea uwezo walinzi wa makampuni ya ulinzi ya kibinafsi ili waweze kushiriki vyema katika kutekeleza majukumu yao katika maeneo yao ya kazi," alisema.

Aidha, Kamanda Wendo alitoa salamu za pole kutoka Jeshi la Polisi kwa askari wa kampuni ya SGA aliyepoteza maisha wakati wa tukio la shambulio lililotokea Agosti 25, mwaka huu, maeneo ya ofisi ya Ubalozi wa Ufaransa jijini Dar es Salaam.

Alisema Jeshi la Polisi lilimchukulia ofisa huyo kama sehemu ya jeshi hilo na ndiyo sababu akapewa heshima zote anazostahili kupewa ofisa wa Jeshi la Polisi anapopoteza maisha akiwa kazini na kwamba askari huyo alikuwa ni kielelezo cha kujituma kunakofanywa na wafanyakazi wa makampuni ya ulinzi ya kibinafsi katika kuhakikisha usalama unakuweko ndani ya jamii.

Mkurugenzi Mkuu wa SGA Tanzania, Eric Sambu, alisema kampuni hiyo inaadhimisha miaka 37 ya kufanya kazi Tanzania, ambapo alisema katika kipindi hicho imepata mafanikio makubwa.

"Mafanikio haya yamekuwa makubwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kutokana na mabadiliko ambayo uongozi wa kampuni yetu umefanya, sambamba na ushirikiano ambao tumekuwa tuliupata kutoka kwa wadau mbalimbali likiwamo Jeshi la Polisi," alisema na kuongeza uimarishaji wa wafanyakazi wa kampuni hiyo umewawezesha wafanyakazi wake kufanya kazi na kukidhi ya wateja wao kampuni hiyo.

Alisema mafanikio mengine ya kampuni hiyo pia yametokana na kuwa na wafanyakazi waaminifu, waadilifu na wenyebidii katika kutekeleza majukumu yao.

# Kata kuanza kugawa taulo za kike shuleni

**Na Christina Mwakangale**

KATA ya Saranga iliyopo Jimbo la Ubungo mkoani Dar es Salaam, itaanza kugawa taulo za kike bure kwa Shule ya Sekondari Saranga, kuanzia mwezi huu, ikilenga kuwaondolea vikwazo wasichana shuleni.

Diwani wa Viti Maalumu, Liberatha Samson, amesema wataanza kwa kuchangishana fedha viongozi wa kata hiyo wakiwamo wenyeviti, watendaji na wadau huku wakiandaa andiko kwa Halmashauri ya Ubungo kutenga bajeti.

Liberatha aliyasema hayo juzi kwenye mafunzo kuhusu bajeti yenye mrengo wa wa kijinsia kwa madiwani, watendaji kata, wenyeviti wa serikali za mitaa kutoka Kata ya Saranga na Mabwepande, mkoani Dar es Salaam.

Alisema mafunzo hayo yametoa mwanga na tafakuri kwa viongozi wa mtaa, ili kuanza kutatua matatizo ya wananchi wao wenyewe kwa kuweka mikakati, badala ya kusubiri bajeti kuu ya serikali.

"Mimi nipo kwenye kamati za huduma za jamii tunazo changamoto nyingi shuleni, hasa zikiwakumba wasichana shuleni kutokana na idadi ndogo ya vyoo, maji, kukosa taulo za kike. Sasa kuanzia Oktoba, tutatoa taulo za kike na baadae kujadili kutengwa bajeti maalumu kutoka halmashauri," alisema Liberatha.

Awali, Shakila Mayumana akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambao wanaratibu mafunzo kwa kushirikiana na COADY International, alisema utendaji wa mzuri wa kiongozi ni ule unaoacha alama katika jamii.

Alisema viongozi wanaoleta mabadiliko kwenye jamii hukumbukwa kwa sababu utatuzi wa matatizo ya wananchi husaidia kuwainua kiuchumi ikiwamo kupunguza umaskini.

"Mafunzo haya yanajenga uelewa wa pamoja kwa viongozi, jamii juu ya umuhimu wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia na kupitia bajeti za kata, halmashauri kwa kuzingatia jinsia, vipaumbele," alisema Shakila.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Deogratius Temba, alisema bajeti yenye mrengo wa kijinsia huondoa migogoro, kuleta usawa, kuondoa mfumo dume pamoja na ukatili wa kijinsia.

## HABARI KITAIFA

# Walivyonusurika kifo nyumba ikiteketea

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

FAMILIA ya mtumishi Idara ya Uhamiaji mkoani Shinyanga, Mwinji Nyombo, wamenusurika kifo baada ya nyumba ambayo wamepanga katika Mtaa wa Viwanja vya Mwadui Ndembezi Manispaa ya Shinyanga kuteketea kwa moto.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya usiku wakati wanafamilia hao wanane wakiwa wote nyumbani baadhi wakila chakula sebuleni, wengine wakiwa vyumbani, huku htumishi huyo wa Uhamiaji akifanya mazoezi chumbani kwake.

Nyombo akizungumza na Nipashe, alisema wakati akiendelea kufanya mazoezi, ghafla akasikia kelele za mdogo wake akisema watoke nje haraka nyumba yao inawaka moto na moshi umeshatanda, ndipo wote wakakimbilia nje na kunusurika kifo.

"Moto huu ulianza kuwaka kwenye chumba cha wavulana, na baada ya kutoka nje tukaanza kuomba msaada kwa majirani kuuzima, na jinsi ulivyokuwa kuuzima kwa maji na mchanga usingewezekana, ndipo tukaanza taratibu za kuomba msaada Jeshi la Zimamoto, lakini wamechelewa kufika na nyumba imeteketea yote, ila tuna shukuru wote tupo wazima," alisema Nyombo.

Naye shuhuda wa tukio hilo, Projesta Galumanzi, alisema baada ya kusikia kelele, wakafika kwenye nyumba hiyo kutoa msaada na kukuta moto mkubwa, ndipo wakaanza kujaribu kuokoa baadhi ya vitu, na kukomea kutoa makochi na TV tu, huku vitu vingine vyote vikiteketea.

Kwa upande wake Ofisa Opresheni wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Shinyanga, Inspekta Edward Lukuba, alisema walichelewa kufika eneo la tukio sababu gari lao la kuzimia moto ni bovu, na wana gari moja tu, ambapo ilibidi waazime kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kambi ya Kizumbi, ndipo wakafika na kuuzima moto huo.

Aidha, alisema chanzo cha moto huo ni hitilafu ya mfumo wa umeme ndani ya nyumba hiyo.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi na Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi, Aikansia Muro, wakipeperusha bendera kwa kuzindua rasmi promosheni ya Bonge la Mpango awamu ya pili iliyozinduliwa jijini Dar es Salaam ikiwa na lengo la kuhamasisha nidhamu ya kuweka akiba kwa wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa dini waombwa kutoa elimu ya corona

**Na Said Hamdani,** LINDI

VIONGOZI wa dini mkoani Lindi, wameombwa kutumia nyumba zao za ibada kusaidia na kuelimisha jamii umuhimu wa kupatiwa chanjo kujikinga na ugonjwa wa corona.

Mkuu wa Mkoa huo, Zainabu Rajabu Telack, alitoa ombi hilo, wakati anazindua mpango shirikishi na uharakishaji kamati ya Afya ya msingi {PHC} namna chanjo itakavyofikishwa kwa wananchi katika kuwapatia huduma hiyo.

Alisema ugonjwa huo ni hatari, kwani una madhara makubwa, yakiwamo ya kiuchumi, kupunguza nguvu kazi ya Taifa, kuongezeka kwa gharama za matibabu na idadi ya vifo vya watu katika mataifa mbalimbali.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema jamii kukosa uwelewa wa kutosha juu ya umuhimu watu kupata chanjo, kunasababisha wananchi wengi kutojitokeza kwa wingi kwenda vituo vya kutolea huduma kupata chanjo ili waendelee kuwa salama.

"Viongozi wetu wa dini ebu mtusaidie kuwaelimisha waumini wenu, ikizingatia wengi wenu tulikuwa wote kupata chanjo Agost 3, mwaka huu," aliongeza.

Alisema serikali imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha unadhibitiwa kwa kuagiza dawa nje ya nchi na jamii kupatiwa elimu ya kujikinga, ikiwamo kuosha mikono kutumia maji tiririka na sabuni, vitakasa mikono, kuepuka mikusanyiko na kuvaa barakoa.

"Haya mambo ya kuvaa barakoa kila uchwao yataisha pale wananchi wote watakapokuwa wamechanja

Awali akitoa taarifa fupi katika kikao hicho, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Dk. Kheri Kagya, alisema katika kuhakikisha jamii yote inafikiwa kupata huduma hiyo, ameandaa vituo 143 na timu ya wataalamu 138 watakaopita nyumba hadi nyumba kuwapa wananchi elimu na chanjo.

Dk. Kagya alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kila mwananchi anayestahili kuchanjwa anapata huduma hiyo.

# Watumishi wanaowaomba rushwa w'biashara waonywa

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amewaonya watumishi wa umma wanaowasumbua wafanyabiashara na wawekezaji kwa kuwaomba rushwa ili kunyoosha mambo yao.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki na kuwataka watumishi hao kukaa kando na rushwa badala yake wawe mstari wa mbele kuwasaidia wafanyabiashara wote wanaotaka kufanya biashara ama kuwekeza mkoani humo.

Gabriel alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa kampuni ya usafirishaji wa mizigo kutoka China, Dubai kuja Tanzania ya Silent Ocean uliofanyika mkoani humo katika ofisi ya GSM.

Aliwataka wafanyabiashara watakaopatwa na adha hiyo watoe taarifa ofisini kwake kwani Mwanza ni sehemu sahihi ya biashara hivyo anawakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara mbalimbali kuwekeza katika sekta ya kilimo, biashara, utalii, ujenzi, elimu, ufugaji na afya.

"Serikali ya mkoa itaendelea kuweka mazingira bora na ya haki kwa kila mfanyabiashara ili kuimarisha uwekezaji na kuhamasisha sekta mbalimbali ikiwemo utalii, hivyo kampuni hii ya usafirishaji mfanye kazi kwa uaminifu ili kuwajengea amani wafanyabiashara," alisema Gabriel.

Naye Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Mohamed Soloka, alisema kuwa wameamua kufungua tawi mkoani Mwanza kutokana na uhitaji wa wafanyabiashara waliokuwa wakifuata bidhaa Dar es Salaam, hivyo wamewaondolea adha hiyo.


Aliongeza kuwa mizigo yote itasafirishwa katika hali nzuri hivyo ni wakati wa wafanyabiashara kuchangamkia fursa hiyo pia njia hiyo itaongeza pato la serikali kupitia kodi kwa kuwa wafanyabiashara wataongezeka.

Naye Mkuu wa Masoko na Mauzo wa kampuni hiyo, Mohamed Kamilagwa, alisema itawapunguzia wafanyabiashara usumbufu wa kusafirisha biashara kutoka China na Dubai kuja Mwanza.

"Mteja atasaidiwa kupunguza usumbufu wa kuulizia mzigo kutoka Dar es Salaam, lakini wale waafnyabiashara tulionao itawarahisishia kuwapunguzia gharama za kusafirisha, usumbufu wa kuuliza na kuokoa mda ," alisema Kamilagwa.

Mfanyabiashara katika jiji la Mwanza, Betty Mgema alisema kampuni hilyo ltawasaidia wao katika kusafirisha mizigo kutoka China na Dubai kwenda Mwanza kwani itatupunguzia gharama ya kusafiri na muda.

Nipashe
Spotika



KIKOSI BORA CHA USAJILI MPYA MSIMU 2021/22 UK. 12 - 13

# MABEKI WA KATI WA5 WANAONG'ARA ULAYA

## ISIKUPITE

TANGU msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2021/22 kuanza na kuchezwa mechi mbili kwa kila timu hadi sasa, Klabu ya Simba ndiyo inayoongoza kuandamwa na majeruhi (5); Sadio Kanoute, Shomari Kapombe, Joash Onyango, Thadeo Lwanga na Kennedy Juma.



**LONDON,** England

MPIRA wa miguu ni mchezo ambao mara nyingi huelezewa kama wenye idadi ya chini ya kufunga mabao. Kwa kuzingatia hali yake ya ushindani mkubwa, inamaanisha walinzi wa kati huunda sehemu ya msingi ya mchezo huo.

Kwa msimamo wao katikati ya ulinzi wa timu, ni jukumu la beki wa kati kuizuia timu yake kufungwa mabao. Lakini katika mchezo wa kisasa, jukumu lao limebadilika sana.

Mabeki wa kati hawaonekani tena kama kinga nyuma. Wanatumikia pia kuanzisha shambulio. Walinzi wa katikati hawaruhusiwi kukaa tu wakati mashambulizi yanaposukumizwa mbele.

Katika mchezo wa kisasa, ni jukumu la beki wa kati kurekebisha safu zao kila wakati ili kuzuia vitisho vyovyote vya shambulio la kushtukiza. Kwa kuongezea, mabeki wa katikati wanaunda safu ya mwisho ya ulinzi. Kwa kucheza safu ya juu, pia wanaunda shinikizo kubwa kwa wapinzani na kuongeza shambulio la timu.

Kushuka na kupanda katika kusaidia mashambulizi wakianzia nyuma. Hizi ni kazi za kujihami ambazo ni za msingi kwa ufafanuzi wa mlinzi wa kisasa.

Makala haya yanawaangalia walinzi watano bora kwa sasa katika ligi tano kubwa Ulaya, hawa hapa...

### #5. SIMON KJÆR

Simon Kjær ni mchezaji mzoefu wa AC Milan ambaye kwa sasa anaonyesha kuwa kwenye kiwango bora na imara kwa timu yake. Kjær amekuwa na mabadiliko makubwa ya kiwango chake tangu alipofunga bao dhidi ya miamba Manchester United kwenye Ligi ya Europa. Kiwango chake kilimwezesha kupata nafasi kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Denmark kwenye michuano ya Euro 2020. Sasa, yeye pia ni mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwenye safu ya ulinzi ya AC Milan yenye chaguzi kama Fikayo Tomori na Alessio Romagnoli.

Kjær katika mechi nne za Milan katika msimu huu, ameisaidia timu yake kutoruhusu bao katika mechi tatu. Milan pia ina moja ya ulinzi mkali zaidi huko Ulaya.

### #4. JULES KOUNDÉ

Mfaransa huyu mwenye umri wa miaka 22, Jules Koundé, anaonekana kuwa katika kiwango bora msimu huu. Mapema kwenye dirisha la uhamisho, Chelsea ilijaribu kupata huduma yake, lakini ilishindwa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho. Sevilla ilikataa jaribio lao, kwani halikutimiza hesabu yao wanayoihitaji kumwachia mchezaji huyo. Koundé hakika ameweka sakata hilo nyuma na sasa yupo kwenye msimu mpya na Sevilla.

Kwa ujasiri mpya, hadi sasa amekuwa na kiwango bora zaidi kwenye ligi. Katika mechi nne kwenye msimu wa sasa, tayari amecheza mechi tatu bila kuruhusu bao. Pia ameshinda mechi nne na kuwa na uwezo mkubwa zaidi kwa kuzuia mashambulizi kwa asilimia 90.5.

### #3. RÚBEN DIAS

Rùben Dias wa Manchester City ni mchezaji mwingine ambaye anafurahia mwanzo mzuri wa msimu. Ingawa, Manchester City bado hawajafika kwenye kilele cha Ligi Kuu, Dias amechukua jukumu kubwa katika mechi tano bila kuruhusu bao, shukrani zote kwa huduma yake, City wameruhusu bao moja tu kwenye ligi hadi sasa.

Kwa sasa Dias anafurahia kiwango cha kuzuia kwa asilimia 93.9.

### #2. VIRGIL VAN DIJK

Baada ya Virgil van Dijk kukosa karibia kipindi chote cha msimu uliopita kutokana na jeraha la goti, amerudi na amejiandaa kuthibitisha ubora wake vizuri zaidi msimu huu. Kufikia sasa amecheza mechi nne bila kuruhusu bao kwa Liverpool kwenye Ligi Kuu England. Kiwango chake pia kimechangia Liverpool kupata alama 13 na hadi sasa wao ni viongozi wa Ligi Kuu (kabla ya mechi za juzi na jana)

Van Dijk anajivunia kukamilisha pasi kwa asilimia 91.

### #1. ANTONIO RÜDIGER

Antonio Rüdiger ni mchezaji ambaye ni injini ya ulinzi wa Chelsea. Chini ya kocha Thomas Tuchel, Chelsea imeonekana kuwa na safu ya ulinzi imara zaidi.

Katika kipindi chote cha utawala wa Tuchel, Chelsea wameunda safu nzuri ya takwimu za kujihami. Katika kampeni ya sasa, Chelsea hawajaruhusu mabao mengi zaidi kutikisa kwenye nyavu zao.

Rüdiger ameisaidia Chelsea kucheza mechi nne bila kuruhusu bao katika mechi tano za Ligi Kuu. Yeye pia anafurahia asilimia 89.7 ya kuokoa hatari langoni mwake. Hadi sasa (kabla ya mechi za jana na juzi) Chelsea imeruhusu mabao mawili tu kwenye ligi. Rudiger ndiye mlinzi wa kiwango cha juu zaidi hadi sasa kwenye ligi tano bora huko Ulaya.



ANTONIO RÜDIGER

Extra Time

# KIKOSI BORA CHA USAJILI MPYA 2021/22



RONALDO

**LONDON,** England

PAMOJA na hasara za kifedha kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19 kuanza kupungua, klabu nyingi ziliimarisha safu zao msimu huu wa majira ya joto. Wakati uhamisho wa bure ulibaki kama njia ya biashara inayopendelewa, klabu pia ziligawanyika kupata malengo yao ya juu ya uhamisho wa wachezaji.

**Msimu wa majira ya joto uliona wachezaji wengi wenye majina makubwa wakibadilisha klabu.**

Kwa kutaja wachache, Cristiano Ronaldo alirudi Manchester United, wakati Lionel Messi na Sergio Ramos walijiunga na PSG, wakati huo huo, David Alaba alihamia Real Madrid, huku Antoine Griezmann akirudi Atletico Madrid.

Wakati wachezaji kama Griezmann wakichukua muda wa kuanza kurudisha kiwango chake, wageni wengine wapya wamepiga mbio.

Kwenye makala haya hapa tunaangalia kikosi cha wachezaji wageni 11 kinachofanya vizuri. Uundwaji wa kikosi hiki umezingatia mfumo wa 4-3-3, twende sasa...

### # GOLIKIPA - MIKE MAIGNAN (AC MILAN)

Mike Maignan amekuwa mmoja wa makipa wenye kiwango bora zaidi msimu huu. Baada ya kucheza mechi 21 bila kuruhusu bao wakati Lille ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu Ufaransa msimu uliopita, raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na AC Milan.

Ni siku za mapema, lakini Maignan tayari amewavutia waajiri wake wapya. Amekuwa na mechi tatu ambazo hajaruhusu bao kwenye michezo mitano ya Serie A na kuwasaidia Rossoneri hao kuongoza kwa alama mbili zaidi ya Napoli kwenye msimamo wa ligi.

Ingawa safari yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ilisababisha Milan kurudi kutoka Anfield na kichapo cha 3-2, Maignan alikuwa mmoja wa wachezaji nyota wa klabu hiyo. Aliwashtua wenyeji mara kadhaa kabla ya kipindi cha pili kuona Liverpool inachukua alama zote tatu.

Maignan anatarajia kuendelea na kiwango chake cha kupendeza wakati Milan inataka kurudi kwenye siku zake za kushinda taji la kwanza la Serie A tangu mwaka 2011.

### # BEKI WA KUSHOTO - DAVID ALABA (REAL MADRID)

David Alaba ni mmoja wa walinzi bora kabisa kwenye mchezo huo kwa sasa. Baada ya kipindi kizuri cha miaka kumi kule Bayern Munich, ambapo alishinda mataji ya kutosha, Alaba alitua Real Madrid kwa uhamisho wa bure.

Akirithi jezi namba nne kutoka kwa nahodha wa klabu hiyo anayeondoka, Sergio Ramos, Alaba amevutia katika michezo sita kwenye mashindano yote ambayo amecheza msimu huu. Kurudi kwenye jukumu lake la kucheza beki ya kushoto nafasi anayoipenda zaidi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, tayari ametoa asisti mbili.

Baada ya kuondoka kwa walinzi wa kati, Ramos na Raphael Varane, Alaba amebakia kuwa mmoja wa walinzi wenye uzoefu wa Madrid. Ataonekana kuchukua jukumu muhimu wakati klabu hiyo inahitaji kushinda mataji makubwa msimu huu.

### # MLINZI WA KATI - ODILON KOSSOUNOU (BAYER LEVERKUSEN)

Odilon Koussounou ni mmoja wa mabeki wa kati wanaofurahisha zaidi kwenye mchezo huo kwa sasa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 20, alifurahia kampeni ya kusimama vizuri katika klabu ya Club Brugge msimu uliopita, akifurahisha na uwezo wake kwenye mipira ya mwisho. Hiyo ilisababisha Bayer 04 Leverkusen kuisaka saini ya Koussounou, ambaye amekuwa na mwanzo mzuri pale kwenye dimba la BayArena. Koussounou ameshatoa asisti moja kwenye mchezo wake wa kwanza pale Leverkusen.

Ingawa bado hajafungua akaunti yake ya mabao kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Leverkusen inatarajia Koussounou kuendelea kuwa kwenye kiwango bora wakati wanatafuta kuwania taji la ligi. Baada ya michezo mitano, Leverkusen wameachwa alama tatu na vinara Bayern Munich.

### # MLINZI WA KATI - RAPHAEL VARANE (MANCHESTER UNITED)

Raphael Varane ni mmoja wa walinzi bora wa kati wa kucheza mpira kwenye mchezo huo. Baada ya kipindi kizuri cha miaka kumi kule Real Madrid, mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018 akiwa na Ufaransa, alitua Manchester United msimu huu wa majira ya joto.

Bado ni siku za mapema katika uwanja wake wa Old Trafford, lakini Varane tayari ameshapata ushirikiano mzuri na nahodha wa klabu hiyo, Harry Maguire. Mfaransa huyo amevutia pande zote mbili, akifanya vitu muhimu na kutoa asisti kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu England.

Varane atatafuta kuendelea na maisha yake mazuri huko Old Trafford wakati United inatafuta taji lao la kwanza la Ligi Kuu kwa karibu muongo mmoja.

### # BEKI WA KULIA - ACHRAF HAKIMI (PSG)

Achraf Hakimi amekuwa na wakati mzuri PSG, akifunga bao kwenye mechi yake ya kwanza ya klabu hiyo baada ya msimu mzuri kwa washindi wa Serie A wa msimu uliopita, Inter Milan.

Moja ya walinzi bora zaidi wa pembeni kwa sasa, Hakimi amekuwa moja ya majina ya kwanza kwenye orodha ya timu kwenye kikosi cha PSG chenye nyota kibao. Tayari ameshafunga mara tatu, pamoja na ushindi wa dakika za mwisho, na kutoa asisti mbili. Hiyo imesaidia PSG kupata alama saba zaidi kileleni baada ya michezo saba tu.

Huku PSG ikiwa tayari ina nafasi ya kulitwaa taji la Ligue 1, Hakimi sasa atatafuta kuisaidia timu yake mpya kushinda taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### # KIUNGO WA KUSHOTO - JACK GREALISH (MANCHESTER CITY)

Jack Grealish alikuwa mchezaji ghali zaidi wa Kiingereza katika historia wakati Manchester City ilipotoa euro milioni 117.5 kumsajili.

Kiungo huyo alifunga mara ya kwanza nyumbani kwa City na pia alitikisa nyavu katika mechi yake ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Katika michezo saba kwenye mashindano yote, ametoa mchango wa mabao manne (mabao mawili, asisti mbili).

### # KIUNGO WA KATI MSHAMBULIAJI - MARTIN ODEGAARD (ARSENAL)

Raia huyu wa Norway hakuwa na wakati mzuri kule Real Madrid miaka kadhaa iliyopita. Lakini ukosefu wa nafasi za kutosha kwenye kikosi cha kwanza ilimaanisha Odegaard alilazimika kutafuta malisho mapya. Baada ya kuvutia huko Arsenal wakati wa kipindi cha mkopo msimu uliopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amesajiliwa kwa mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto.

Odegaard alifunga kwa mpira wa adhabu ndogo dhidi ya Burnley wakati 'Washikabunduki' hao walipopata ushindi wao wa pili baada ya kuanza msimu na kupoteza mechi tatu mfululizo.

### # WINGA WA KULIA - HAKAN CALHANOGLU (INTER MILAN)

Hakan Calhangolu amekuwa na wakati mzuri kule Inter Milan. Kiungo huyo alifunga na kutoa asisti kwenye mechi yake ya kwanza ya Serie A na klabu yake mpya, ambayo iliwaacha nyota wake kadhaa kabla ya kuanza kwa msimu huu ili kupunguza shida zao za kifedha.

Calhanoglu amewasili Inter baada ya msimu mzuri kule Milan. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uturuki alifunga mara nne na kutoa asisti kumi kuwasaidia Rossoneri kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka saba msimu uliopita.

### # WINGA WA KUSHOTO - CRISTIANO RONALDO (MANCHESTER UNITED)

Cristiano Ronaldo alirudi kufunga mabao pale Manchester United baada ya misimu tisa kule Real Madrid na mitatu Juventus.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 36, alifunga kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu baada ya kurudi hapo kwa kipindi cha miaka 12. Baada ya kufunga kwenye mchezo wa kwanza wa United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati ikichezea kichapo kutoka kwa Young Boys, Ronaldo alifunga kwenye mchezo wake tatu mfululizo wikendi iliyopita.

### # MSHAMBULIAJI WA KATI - ROMELU LUKAKU (CHELSEA)

Romelu Lukaku ni mmoja wa washambuliaji moto zaidi kwenye sayari hii kwa sasa. Amewasili Stamford Bridge kwa uhamisho wa euro milioni 115 kutoka Inter Milan.

Lukaku, kama Ronaldo, alifunga katika mechi yake ya kwanza kurudi kwenye klabu yake ya zamani wakati Chelsea ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Arsenal. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, sasa amefunga mara tatu katika michezo minne ya Ligi Kuu. Lukaku pia aliifungia Chelsea kwenye ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Zenit St. Petersburg katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, amewasili Chelsea baada ya kampeni kubwa na washindi wa Serie A Inter Milan. Lukaku alifunga mabao 24 ya ligi wakati Inter Milan ilishinda taji lao la kwanza la ligi kwa kipindi cha miaka 11, msimu uliopita.

### # WINGA WA KULIA - MEMPHIS DEPAY (BARCELONA)

Memphis Depay ameanza maisha ya kupendeza pale Barcelona. Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United amekuwa na wakati mzuri Camp Nou baada ya kukaa sana Olympique Lyon.

Depay amefunga mabao mawili na kutoa asisti katika michezo mitano ingawa Barcelona wameanza msimu huu wakiwa bila Lionel Messi.

Mholanzi huyo, hata hivyo, alishindwa kutamba kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona. Depay aliambulia patupu wakati Blaugrana hao wakichapwa mabao 3-0 na Bayern Munich nyumbani na baadaye idadi kama hiyo ya mabao kutoka kwa Benfica.

## Nukuu

"Ahadi zinazotolewa kuongeza motisha zinaharibu mpira, hazina maana yoyote, kama huna uwezo huna tu. Kwa nini zitolewe wanapokutana na Simba tu? Zinavuruga mpira, zinasababisha matumizi ya nguvu yasiyostahili na kutumizia wachezaji kama ambavyo imetokea dhidi ya Dodoma Jiji na Biashara United," **Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Crescentius Magori.**




"Kufuatia mamlaka aliyopewa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura ya 357 (Rejeo la 2002), baada ya kupokea ombi lililoletwa kwake na TFF, amempa uraia wa Tanzania Mchezaji wa Mpira wa Miguu, Kibu Denis Prosper, Sept. 30, (mwaka huu)," **Wiraza ya Mambo ya Ndani.**



"Tumejua aina ya ligi ambayo tutacheza msimu huu, hii ligi itakuwa ni kama vita, lakini nina uhakika Simba imejipanga, tunacheza mechi ngumu sana, tuko tayari kupambana na hilo ndilo naweza kusema, najivunia sana wachezaji wangu," **Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes.**





Winga wa Simba, Peter Banda, akiwalamba chenga mabeki wa Biashara United kwenye moja kati ya mechi nane za ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, timu hizo zilitoka suluhu kwenye Uwanja wa Karume mkoani Mara. **PICHA: MAKTABA**

# MAMBO 5 USIYOYAJUA UFUNGUZI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ilivyotarajiwa, Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 tayari umeanza na kwa michezo miwili kwa kila timu, hakika zimeonekana zimejiandaa kisawasawa.

Hakuna timu yoyote iliyoshinda zaidi ya mabao mawili kwenye mechi za ufunguzi na ni timu mbili tu zilizofanya hivyo, kabla ya mechi za jana jioni. Kwenye mechi za ufunguzi, Namungo FC iliichapa Geita Gold mabao 2-0, huku ushindi kama huo ikiupata Polisi Tanzania dhidi ya KMC.

Mbeya Kwanza iliichapa Mtibwa Sugar bao 1-0, Dodoma Jiji ikiidungua Ruvu Shooting 1-0, Mbeya City ikipata ushindi kama huo dhidi ya Prisons, huku Yanga nayo ikishinda idadi hiyo ya goli dhidi ya Kagera Sugar. Sare zilikuwa mbili tu kwenye mechi za ufunguzi, Coastal Union ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC, Biashara na Simba zikitoka suluhu.

Hata kwenye mechi chache za raundi ya pili, hali ilikuwa ngumu kwa timu zote, Simba ikifunga Dodoma Jiji bao 1-0, Yanga ikiidungua Geita Gold idadi kama hiyo ya watani zao, Ruvu Shooting nayo ikiibamiza Biashara United bao 1-0, Polisi Tanzania ikiisulubu Azam FC mabao 2-1.

Katika makala haya tumekusanya rekodi na takwimu mbalimbali zilizojitokeza kwenye mechi hizo nane za ufunguzi, ambazo ni za raundi ya kwanza msimu huu.

**#1. SIMBA YASHINDWA KUPATA BAO**

Suluhu ya bila kufungana ambayo Simba iliipata Jumanne iliyopita dhidi ya Biashara United, imeifanya timu hiyo kushindwa kupata bao kwenye mechi ya ufunguzi kwa mara ya kwanza baada ya misimu 13.

Mara ya mwisho Simba kutofunga bao mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni msimu wa 2007/08, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Septemba 23, 2007, kwa bao lililofungwa na Sunday Peter.

Kwa misimu yote 13 iliyofuata, Simba ilikuwa ikifunga bao moja au zaidi kwenye mechi zote za ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hata mechi ambazo ilikuwa ikitoa sare, hadi Jumanne iliyopita iliposhindwa kufanya hivyo kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

**#2. YANGA YATOA MKOSI**

Yanga imepata ushindi kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya ufunguzi baada ya misimu miwili. Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera Jumatano iliyopita, umemaliza misimu miwili ya mikosi kwa timu hiyo.

Msimu wa mwisho Yanga kushinda mechi ya ufunguzi ilikuwa ni 2018/19 ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1. Lakini msimu wa 2019/20 ilianza ligi kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na msimu uliopita ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Prisons, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**#3. MKWAKWANI KAA LA MOTO KWA AZAM FC**

Bao lililofungwa na Hance Masoud dakika moja kabla ya mechi kumalizika, liliendeleza rekodi mbaya ya Azam kutoshinda mechi yoyote ile kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya Coastal Union misimu minne mfululizo. Ni baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji, ikiwa inaongoza mpaka dakika ya 89, Hance alipachika bao na kuifanya rekodi hiyo kuendelea kusimama pale pale.

Katika mechi nne ilizocheza Azam FC kwenye Uwanja wa Mkwakwani, tangu Coastal Union ipande daraja na kucheza Ligi Kuu msimu wa 2018/19, Azam imetoka sare mbili na kufungwa mara mbili. Msimu wa wa 2018/19 iliambulia sare ya bao 1-1, kabla ya kuchapwa bao 1-0 msimu uliofuata wa 2019/20. Azam ilichapwa tena mabao 2-1 msimu uliopita kwenye uwanja.

**#4. MTIBWA BADO MAJANGA UFUNGUZI**

Kwa misimu minne sasa, Mtibwa Sugar haijapata ushindi kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu. Hii ni baada ya kukumbana na kipigo cha bao 1-0 Jumatano iliyopita dhidi ya Mbeya Kwanza, Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani. Mara ya mwisho Mtibwa kupata ushindi ugenini ilikuwa msimu wa 2017/18 ikiichapa Stand United bao 1-0 kupitia kwa Huusein Javu.

Baada ya hapo ni tabu tupu, kwani msimu uliofuata 2018/19 ikachapwa mabao 2-1 dhidi ya Yanga, ikapoteza tena 3-1 dhidi ya Lipuli msimu wa 2019/20, huku msimu uliopita ikitoka suluhu ya bila kufungana dhidi ya Ruvu Shooting.

**#5. SIMBA HAIJAPOTEZA MISIMU 14**

Pamoja na suluhu dhidi ya Biashara, Simba imeendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi yoyote ya ufunguzi kwenye Ligi Kuu kwa msimu wa 14 mfululizo tangu msimu wa 2008/09, ambapo imeshinda mechi 11 na kutoka sare mara tatu.

Mara ya mwisho ilikuwa ni msimu wa 2007/08, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Septemba 23, 2007, kwa bao lililofungwa na Sunday Peter.

Sare ya Jumanne iliyopita ilikuwa ni ya tatu kwa timu hiyo kwa msimu wa 14, zingine zikiwa ni za mabao 2-2 dhidi ya Rhino Ranger ya Tabora msimu wa 2013/14 na sare kama hiyo msimu uliofuata 2014/15 dhidi ya Coastal Union.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI Mnigeria Yakubu Ayegbeni, ni mchezaji wa kwanza kutoka barani Afrika kufunga hat-trick, akifanya hivyo wakati Maccaibi Haifa ikiichapa Olympiacos mabao 3-0 mwaka 2002 katika hatua ya makundi ya michuano hiyo. Kwa sasa anaichezea Coventry City ya England.



# Wafugaji watakiwa kujitokeza kuhesabiwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

JAMII ya wafungaji wenye tabia ya kuhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho ya mifugo wametakiwa kutoa ushirikiano kwa serikali kuhusu sensa ya watu na wakazi itakapofanyika ili wahesabiwe kwa usahihi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano mkoani Dodoma, Evance Chande, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu zoezi hilo mwakani.

Chande, alitoa ushauri huo kutokana na jamii hiyo kuwa na tabia ya kuhamahama, suala ambalo linaweza kusababisha kukosa fursa ya kushiriki kikamilifu zoezi hilo.

Alisema ili kupata takwimu sahihi za sensa ya watu na makazi kwa jamii hiyo ya wafungaji ambao baadhi yao huishi kwa kuhamahama wanatakiwa kutoa ushirikiano mkubwa kwa majibu yaliyo sahihi yatakayowezesha serikali kupanga mipango yake ya maendeleo.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo aliiomba serikali kuzifikia jamii hizo za wafugaji kwa wakati ili kutoa elimu itakayohamasisha kuhesabiwa kwenye sensa hiyo ambayo itakayofanyika Agosti 2022.

Alisema elimu hiyo ikiwafikia kwa wakati wataweza kushiriki kwa uaminifu katika kuhakikisha watu wote wa jamii hiyo wanahesabiwa.

"Jamii hiyo ikipatiwa elimu ya kutosha serikali itapata takwimu sahihi, kwa kuwa tayari watakuwa wameelimishwa kwa ajili ya kuhesabiwa, tofauti na wakiachwa bila kuelimishwa wanawezaweza kuhamisha makambi yao wanayoishi," alisema.

Aidha, mwenyekiti huyo aliiomba serikali kutoa elimu ya sensa ya watu na makazi, pia kwa jamii ya wavuvi walipo kwenye makambi ambao na wao wamekuwa na tabia ya kuhamahama kutafuta samaki.

"Kama ilivyo kwa wafugaji kuwa na tabia ya kuhamahama pia na wavuvi na wao ambao wanaoishi kwenye makambi wamekuwa na tabia hiyo hivyo na wao wanatakuwa kupewa elimu ili kutoa ushirikiano kwa serikali kwenye zoezi hilo muhimu," alisema.

Alisema mpango wa serikali ni kuleta maendeleo kwa Watanzania wote, hivyo hata wafugaji na wavuvi wenye tabia ya kuhamahama wanatakiwa kuwamo kwenye sensa ya watu na makazi bila kukosa.



Mashekhe na viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA) Kata ya Chang'ombe, jijini Dodoma wakifanya dua kwenye msikiti wa Muccadam unaoendelea kujengwa kwa nguvu za waumini, juzi. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Shekhe ataka vijana kuondoka vijiweni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kutumia nguvu zao kushiriki katika shughuli za maendeleo badala ya kukaa vijiweni na kuinyooshea vidole serikali kuwa haiwapi ajira.

Ushauri huo ulitolewa jana na Shehe wa Kata ya Chang'ombe jijini Dodoma, Ibrahim Kidura, alipokuwa akizungumza na waandishi habari baada ya kushiriki dua na ujenzi wa msikiti wa kisasa wa Mccadam uliopo katika kata hiyo.

Shehe Kidura aliwataka vijana kuhakikisha wanatumia nguvu walizokuwanazo kwenye shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo ujenzi wa nyumba za ibada.

"Vijana ndiyo wenye nguvu wa wanaweza wa kushiriki kikamilifu shughuli mbalimbali za kimaendelo ikiwamo na ujenzi, hivyo ninawaomba vijana kujitokeza kwa wingi pale shughuli hizo zinapojitokeza," alisema Shehe Kidura.

Naye Shehe Husseni Jumbe aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu Kata ya Chang'ombe kuonyesha mfano wa kuchangia mali na fedha kwa ajili ya ujenzi wa msikiti huo badala ya kutegemea watu wa nje.

Shekhe Jumbe, alisema kuwa waumini wa kata hiyo wanawajibu mkubwa wa kuonyesha mfano katika kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati kutokana na michango yao watakavyojitoa.

"Ninawaomba waumini wa kata hii kujitokeza kwa wingi katika kushiriki ujenzi huu wa msikiti, ili uweze kukamilika kwa wakati," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, aliwaomba waumini kutumia nguvu kazi yao ili kupunguza matumizi makubwa ya fedha.

Bashiru, alisema kuwa wakitumia nguvu kazi na kujitoa kwa wingi ujenzi huo utaweza kukamilika kwa wakati.

# World Vision yawezesha wanawake kilimo bora

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la World Vision limetoa mafunzo ya utekelezaji wa kilimo chenye tija kwa wanawake wa Wilaya ya Chemba ili kuhakikisha wanafanya kilimo bora na chenye tija.

Akizungumza wilayani hapa Joseph Kilimba, mmoja wa waratibu wa mafunzo hayo alisema lengo lao ni kuona wanawake wanafanya kilimo chenye tija ambacho kitawainua kiuchumi.

Alisema kuwa wanahitaji kuona kundi hilo linakuwa katika mfumo wa kilimo tofauti na ilivyokuwa zamani kulima kwa mazoea bila tija.

Aidha, alisema wanawake wengi wamejikita katika kilimo cha mbaazi ambacho ni kilimo biashara.

"Tuko mstari wa mbele kuhakikisha kilimo kinakua hivyo tumejipanga kuwainua," alisema Kilimba.

Hata hivyo, alisema mafunzo hayo yewapa manufaa makubwa wanawake kwa sababu hivi sasa wanavuna mbaazi kwa wingi tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema awali walikuwa wakitumia kilimo cha kienyeji, lakini hivi sasa baada ya kupata mafunzo wameamka na wanafanya kilimo biashara.

Akizungumzia kuhusu kilimo cha nyanya alisema kipo imara kwa hivi sasa kutokana na kuwaboreshea wakulima njia bora na sahihi za kilimo biashara.

"Wameshavuna hivi sasa na kuzipeleka sokoni na wameanza maandalizi ya kilimo cha pilipili hoho ambapo tayari wameshaotesha kwenye vitalu," alisema.

Aliwataka wanawake wa wilaya ya hiyo kuangalia fursa zilizpo na wajikike katika kilimo kwa sababu kinalipa.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Aisha Sule, aliishukuru World Vision kutokana na msaada inayowapa kwa sababu bila wao wasingefika walipo.

Alifafanua kuwa hivi sasa wanakikundi ambacho kinafanya vizuri kutokana na kilimo cha nyanya hivyo wanazidi kusonga mbele.

Alisema hivi sasa kikundi chao wako vizuri na wanawashauri wanawake wengine waingie katika kilimo cha mboga.

Hata hivyo, alisema wamejipanga kuendeleza kilimo cha pilipili hoho ambacho wameanza kukifanya wilayani humo.

# CCBRT yaahidi kupunguza vifo vya wajawazito

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

HOSPITALI ya CCBRT imeahidi kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali kuboresha afya za Watanzania na hasa kupunguza vifo vya kinamama wakati wa kujifungua.

Hayo yamesemwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa hospitali hiyo, Brenda Msangi wakati Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea banda la hospitali hiyo kabla ya kufunga mkutano wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) uliofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki.

Brenda alisema hospitali hiyo imeamua kuunga kwa vitendo kauli ya Rais Samia aliyoitoa wakati akihutubia Bunge ambapo katika sekta ya afya alisisitiza kuwa moja ya kipaumbele chake kikubwa ni kupunguza vifo vya mama wakati wa kujifungua.

"Sisi kama CCBRT tunafanya kazi kwa karibu sana na timu ya mkoa ya afya ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa kipindi cha miaka 10 tumeweza kufanya kazi na vituo 22 vya afya vya serikali na tumeweza kupunguza vifo vya kinamama kwa asilimia 47,"alisema.

Lakini Brenda alisema CCBRT inatarajia kufungua jengo maalum litakalokuwa likitoa huduma ya uzazi na kujifungua ambalo litakuwa na vitanda 200.

Wakati huohuo, Mtendaji Mkuu huyo pia ameishukuru serikali kwa kutambua na kuthamini mchango wao baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyoajiri zaidi na kusema kuwa cheti hicho kimewapa motisha sana wa kuendelea kuwahudumia Watanzania.

Alisema ushindi huo wa CCBRT ni kielezo kuwa serikali na Watanzania kwa ujumla wake wanatambua mchango wa hospitali kwa kujali na kuthamini afya za kinamama na mtoto.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Guy Williams (kushoto), akitia saini mkataba wa ugavi kati ya viongozi wa vyama vya msingi vya wakulima wa miwa Kilombero na kiwanda hicho. Katikati ni Mwenyekiti wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima, Onesmo Mwakyambo na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari nchini, Sophia Stanley. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kilombero yatia saini mkataba ugavi na wakulima wa miwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KAMPUNI ya Sukari Kilombero imetia saini mkataba wa ugavi na viongozi wa vyama vya msingi vya wakulima wa miwa wa Kilombero (AMCOS) wenye lengo la kusimamia ugavi wa miwa na uendeshaji wa biashara ya miwa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2021 hadi 2023.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Guy Williams, alisema kuwa mkataba huo ni wa kipekee kwa kuwa unaonyesha umuhimu wa wakulima katika uendeshaji wa biashara ya sukari ambao wamekuwa wakizalisha miwa zaidi ya tani laki sita kwa mwaka.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kutokana na uzalishaji kuongeka shauku ya kampuni hiyo kwa sasa ni kupanua kiwanda hivyo kusainiwa kwa mkataba huo kutasaidia kuongeza imani ya wawekezaji katika mradi upanuzi wa kiwanda. Aidha, alisema kuwa mradi wa upanuzi wa kiwanda ni mradi mkubwa na unatarajia kugharimu Dola milioni 240 za Marekani sawa na Sh. bilioni 571.

"Mkataba huu ni muhimu kwa sababu unatoa uhakika wa uendelevu wa hatua mbalimbali zinazofuata kwa miaka mitano ijayo hasa hatua za uwekezaji na mradi wa upanuzi wa kiwanda," alisema Williams.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya sukari nchini ambaye ni Mwanasheria wa Bodi hiyo, Sophia Stanley, alipongeza uongozi wa kampuni kwa mahusiano mazuri waliyonayo na wakulima ambayo yamepelekea kusainiwa kwa mkataba huu wa ugavi na hata uamuzi wa kupanua kiwanda ambao unalenga kuziba pengo la uzalishaji wa sukari nchini.

Mwanasheria huyo aliahidi kuwa bodi itaendelea kushirikiana na uongozi wa kampuni hiyo katika hatua zote ikiwamo ya upanuzi wa kiwanda hicho na kuwasisitiza wakulima kuzingatia kanuni za kilimo bora cha miwa.

Naye Mwenyekiti wa Vyama vya Wakulima wa miwa Kilombero, Onesmo Mwakyambo, alisema kuwa wanaamini mkataba huo utaongeza manufaa kwa wakulima na hasa baada ya kukamilika kwa upanuzi wa kiwanda ambacho kwa kiasi kikubwa kitategemea uzalishaji wa wakulima.

Mwakyambo alisema kuwa sasa wakulima wa miwa wa Kilombero wana uwezo wa kuzalisha miwa zaidi ya mahitaji ya kiwanda. Kwa mwaka huu vilevile ubora wa miwa umeongezeka kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara ambazo zimerahisisha usafirishaji wa miwa kutoka kwenye mashamba hadi kufika kiwandani na hivo kupunguza masaa ya kuingiza muwa kiwandani baada ya kuvuna.

Awali akitoa taarifa ya uzalishaji Mkurugenzi wa Mahusiano wa kiwanda hicho, Joseph Rugaimukamu, alisema kuwa mkataba huo uliosainiwa ni mwendelezo wa mkataba wa mwaka mmoja ulioisha Machi mwaka huu na hivyo kukamilisha utaratibu wa miaka mitatu.

## Tozo za maegesho kwa Airtel Money

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wametangaza kuzindua rasmi huduma ya kulipia gharama za maegesho kwa kupitia huduma za 'Airtel Money'.

Kutangaza kwa ushirikiano huo kati ya Airtel Money na TARURA ni mwendelezo wa ushirikiano uliopo kati ya Kampuni ya Airtel na Serikali katika kutumia mfumo wa kisasa wa kiteknolojia kufanya malipo ya huduma na bidhaa mbalimbali njia ambayo ni salama, haraka na nafuu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa kutangaza huduma hiyo, Mkurugenzi wa Huduma ya Airtel Money, Isaack Nchunda, alisema hiyo ni moja ya njia rahisi ambayo itawafanya Watanzania kulipia gharama za maegesho kwa urahisi zaidi na popote walipo.

'Kama mnavyojua hivi karibuni serikali ilitangaza malipo ya maegesho kwa njia ya mtandao. Hii imekuwa ni njia rahisi sana kwani kwa serikali itakuwa inapokea moja kwa moja. Na kwa sababu hiyo, leo ni siku nyingine muhimu kwetu kuungana na wenzetu wa TARURA ili kurahishisha malipo ya maegesho," Nchunda alisema.

Alisema serikali ilishaweka mikakati ya kutumia njia ya kisasa katika kufanya malipo ya huduma mbalimbali kwa haraka na usalama na kuzielekeza taasisi zake zote kutumia Mfumo wa Serikali wa malipo kwa njia ya Mtandao GePG.

Alisema kuwa kuunga mkono juhudi za serikali imekuwa ni moja ya agenda kubwa kwetu. Tunaelewa umuhimu wa serikali wa kuhakikisha kuwa malipo yote ya kwenda serikalini yanafanyika kwa mfumo wa GePG. Tutaendelea kushirikiana na taasisi pamoja na mashirika mengine ya serikali kwa ajili ya kutoa suluhisho ili kutimiza haya'.

"Mara baada ya kukamilisha muamala, mteja atapokea ujumbe mfupi wa maneno kuthibitisha malipo yake. Risiti hiyo ya kielektroniki itakuwa ndio uthibitisho wa malipo na ni rahisi kwa kuhifadhi au kwa kufuatilia kwa baadaye kwani haiwezi kupotea au kuharibika," alisema.



# 326 mbaroni tuhuma dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limesema kuwa operesheni maalum ya kupambana na dawa za kulevya imefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 326 waliokamatwa na dawa hizo.

Hayo yalielezwa na Kamishna wa Jeshi hilo, Mohammed Hassan, juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya Polisi Kilimani Mjini Zanzibar.

Alisema operesheni hiyo iliyopewa kwa jina la 'nyangumi' ilianza Agosti 20, mwaka huu katika ukanda wa mwambao wa bahari ambapo kwa Zanzibar imehusisha mikoa yote mitano.

Alisema watuhumiwa hao 326 ni kwa kipindi cha mwezi mmoja kutoka Agosti 20 hadi Septemba 22, mwaka huu.

Akisema katika kesi hizo, 237 zinahusisha heroine, bangi na mirungi.

"Kesi za heroine ni 26 zenye uzito wa kilogramu 16 na ujazo wa gramu 142, bangi 209 ujazo wa kilogramu 602 na ujazo wa gramu 422 na mirungi kesi mbili zenye uzito wa kilogramu 18," alisema.

Alieleza kuwa watuhumiwa hao 326 waliokamatwa wanaume ni 282 na wanawake 44, na kuwataka wananchi kuendelea kulipa Jeshi la Polisi ushirikiano wa dhati katika kuwabaini na kuwafichua wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya pamoja na wahalifu wengine wa makosa ya jinai.

"Jeshi la Polisi linawasisitiza wahalifu wanaojihusisha na biashara hiyo haramu ya dawa za kulevya kuacha mara moja," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kudumisha amani na utulivu uliopo ili kila mmoja apate fursa ya kufanya shughuli mbalimbali kwa maendeleo ya taifa.



Mkurugenzi Mtendaji Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanali Burhani Nassor, akizungumza wakati wa kikao kati ya tume hiyo na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak (wakwanza kulia), wakati wa kikao cha pamoja na wafanyakazi wa tume hiyo ofisini kwao Migombani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman afunguka ujenzi wa barabara Wilaya ya Kati

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali ya Zanzibar imefanya uamuzi ya kujenga daraja na barabara ya Kijiji cha Uzi Wilaya ya Kati Mkoa Kusini kipindi kifupi kijacho ili kuwarahisishia wanakijiji kufuata huduma muhimu maeneo mbalimbali.

Othman aliyasema hayo juzi huko Kijiji cha Uzi alipotoa ufafanuzi kwa wananchi kuhusu hoja mbalimbali za wakazi wa kijiji hicho waliotaka kujua hatua za serikali juu ya ujenzi wa daraja na barabara ya kijiji hicho ambayo imekuwa ikitolewa ahadi na viongozi kwa muda mrefu bila kutekelezwa.

Othman ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT- Wazalendo, aliyekuwa kwenye ziara ya kichama ya kujitambulisha kijijini hapo, aliwaeleza wananchi hao kwamba suala la ujenzi wa barabara limeshawekewa mipango madhubuti ya serikali, na kwamba kazi inatarajiwa kuanza kutokana na uamuzi uliofanywa na serikali.

Alieleza kwamba awali makadirio ya gharama za ujenzi wa daraja hilo zilizowasilishwa serikalini zilionekana kuwa kubwa kuliko uwezo wa serikali, hivyo kupendekezwa kufanywa tathmini upya ya kazi hiyo kwa kuzingatia unafuu wa gharama.

Alisema kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, serikali imeshawaelekeza wataalamu wake kwenda kufanyia tathmini mpya ya gharama za daraja na ujenzi utaanza baada ya kazi hiyo kukamilika.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu, kuwa na subra, kuendeleza umoja na mshikamano, kutovunjika moyo na viongozi wataendelea kutekeleza juhudi za pamoja katika kutafuta maslahi ya wananchi na taifa kwa jumla.

Akizungumzia suala la uchumi wa bluu, alisema kwamba Zanzibar ina rasilimali muhimu ya bahari ambayo hadi sasa haijatumika vyema na kuwafaidisha ipasavyo wananchi kwa shughuli za baharini ukiwamo uvuvi wa bahari kuu.

Aliwataka viongozi na wananchа wa chama hicho kufuata misingi na maadili ya uongozi, kwa kuwa hatua hiyo itasaidia sana kuandaa na kupata viongozi wazuri wa kutumikia nchi katika hatua mbalimbali za kuleta maendeleo.

Alisema ni vyema waendelee kuwa na subira, na kwamba kuwapo kwa serikali ya umoja wa kitaifa kumetokana na changamoto mbalimbali zilizotokea hapo awali.

Aidha, aliwaambia wananchi hao kwamba katika kufanikisha masuala mbalimbali ya ujenzi wa nchi na kuendesha serikali kwa njia yenye utaratibu na ustaarabu bora ni muhimu kuwapo katiba mpya itakayolenga maslahi ya Wanzanzibari kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Kwa upande wao wananchi wa kijiji hicho cha Uzi ambacho kimezungukwa na Bahari katika risala yao iliyosomwa na Katibu wa ACT Mkoa wa Kati Unguja kichama, Omar Khamis, alisema barabara ya kijiji hicho haipitiki kwa muda mrefu na wanaiomba serikali kuijenga ili isaidie kurahisisha usafari na usafirishaji katika shughuli zao za kila siku za maendeleo.

Pia aliiomba serikali ifanye jitihada za kuinua kipato cha wananchi kwa kutengeneza ajira ikiwamo kupandishwa bei ya mwani ili kuwanufaisha wanaojishughulisha na kilimo hicho.

Naye Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, akitoa ufafanuzi kuhusiana na soko na bei ya zao la mwani, alikiri bei ni ndogo na mpango wa serikali ni kuliongeza thamani ili kuwanufaisha zaidi wakulima.

Aidha, alisema kwamba katika jitihada hizo, serikali ina mpango wa kujenga kiwanda kikubwa cha kuchakata mwani pamoja na kuwawezesha wananchi kujenga viwanda vidogo vya kuchakata mwani ili kuwanufaisha wakulima.

## Tume ya Dawa za Kulevya yafundwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI na wafanyakazi wa Tume ya Kitaifa Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, wametakiwa kudumisha nidhamu katika maeneo yao ya kazi na kuhakikisha wanatimiza majukumu yao kwa ufanisi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, aliyasema hayo kwenye kikao cha watendaji na wafanyakazi wa Tume hiyo ikiwa ni mfululizo wa ziara zake katika kutembelea taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Aliwataka watendaji na wafanyakazi hao kusimamia vyema majukumu yao kama yalivyoelekezwa kwenye mpango wa majukumu ya kazi waliopewa na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Dk. Shajak alisema mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanaanzia ofisini, hivyo wana wajibu wa kutunza siri, kuwa waadilifu, watiifu na wazalendo katika kuitumikia serikali ambayo imewaamini na kuwaweka walipo.

Alisema mapambano dhidi ya dawa za kulevya hayatakwisha iwapo hakutakuwa na ushirikiano unaoanzia ndani ya taasisi yenyewe, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuchukuwa tahadhari katika mapambano hayo na ni vita ya wenye fedha wanaoangalia maslahi yao binafsi.

"Isije kufika mahali ukajiona wewe ndiye mtoa habari za ndani, hatutamwonea mtu haya na iwapo mtu anaona hawezi kutunza siri haendani na sheria na taratibu za Tume hii ambayo inaelekea kuwa mamlaka kamili, ajisalimishe mapema milango iko wazi," alisema.

Aliongeza: "Mapambano ya dawa za kulevya ni yetu sote, hakuna ambaye hajaguswa kuanzia mtumiaji mwenyewe, si wazazi, walezi, familia na hata majirani... wote tunaathirika, wizi umekithiri na mambo mengine yasiyo na maadili."

Katibu huyo alisema serikali inatambua changamoto za wafanyakazi hao, lakini zinafanyiwa kazi kwa hatua ikiwamo ufinyu wa ofisi na uhaba wa wafanyakazi ambayo ni masuala ya kiutawala.

Naye Mkurugenzi Mkuu Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kanali Burhani Nassor, alisema Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeshaandaa muswada wa sheria na unasubiri baraka za Serikali ili Tume hio iwe na hadhi ya kuwa mamlaka kamili.

Alisema mamlaka hiyo itakuwa na uwezo wa kisheria wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kupeleka kesi mahakamani wakati tume inafanya kazi za kuratibu na udhibiti wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

# Polisi yanasa mabasi mabovu 30

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limekamata mabasi 30 yakidaiwa kuwa na makosa mbalimbali.

Kamanda wa Kikosi hicho, Malege Kilakala, aliyabainisha hayo alipofanya ukaguzi katika kituo cha mabasi cha Kahama.

"Tumekuta asilimia kubwa ya mabasi ni mabovu ambayo idadi yake ni 25 na tumeyapiga faini na kuyaruhusu kuendelea na safari, huku mengine matano yakiwa na makosa makubwa ambayo yanahatarisha maisha ya abiria na tumeyazuia kuondoka," alisema Kamanda Kilakala.

Akizungumza na waandishi wa habari, kituoni hapo, alisema licha ya kuyakagua magari hayo, lakini wanatoa elimu mbalimbali kwa abiria kuhusu usalama wao wanapokuwa safarini.

Malege alisema katika operesheni hiyo wanaangalia pia ubora wa mabasi ambayo yanasafiri kwenda katika safari za ndani ya nchi na zile za nje ya nchi na kuongeza kuwa wanakagua mifumo yenye hitilafu na kutoa maelekezo kwa wamiliki wa mabasi hayo.

Alisema wanaangalia usalama wa abiria, lengo ni kuona abiria wanasafiri salama na kuangalia matendo ambayo yanakwenda kinyume cha kanuni za usalama barabarani na kuchukua hatua kwa madereva wazembe.

Hata hivyo, Malege Kilakala alitoa wito kwa wamiliki wa mabasi kuhakikisha kuwa chombo kinakuwa bora ndipo kiruhusiwe kuingia barabarani pamoja na kuona mifumo ya taa, bodi na injini kuwa ni bora na kuongeza kuwa ukaguzi huo utakuwa endelevu. Kwa upande wao abiria waliokuwapo katika baadhi ya mabasi wakisafiri kwenda mikoa mbalimbali walisema kuwa zoezi hilo ni muhimu na ni bora likawa endelevu kwani hakuna abiria ambaye hapendi kufika salama anakopwenda.

Johnson Kayambo, aliyekuwa akisafiri kutoka Kahama kwenda Kibondo mkoani Kigoma, alisema mabasi mengi ni mabovu na kuongeza kuwa ukaguzi huo unaweza muwafanya hata abiria kuwa na imani na gari analokuwa akipanda kwa kuwa litakuwa limekaguliwa na mamlaka husika.



Mwezeshaji wa mjadala uitwao 'Kilinge cha Simulizi' wa kujadili uongozi na masuala ya kijinsia kwenye mitandao ya kijamii, Sadaka Gandi, akiendesha mjadala huo uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania, Mabibo Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Matumizi ya stempu kwenye bidhaa yalivyopaisha mapato

**Na Romana Mallya**

MSIMAMIZI wa Mradi wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETS) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Innocent Minja, amesema katika kipindi cha miezi 30 makusanyo ya kodi ya ushuru wa bidhaa yameongezeka zaidi kutoka Sh. bilioni 297.2 mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 476.7 Juni mwaka huu.

Minja aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa serikali ilitangaza mpango wa kuanzisha ETS Juni mwaka 2018 na awamu ya kwanza ya mradi ilifanyika Januari 15, mwaka 2019 ambapo stempu ziliwekwa kwenye kampuni zinazozalisha bia, pombe na mvinyo.

Alisema awamu ya pili ya mradi huo ilianza Agosti 1, mwaka 2019 wakati stempu za ETS zikibandikwa juu ya maji yenye ladha na vinywaji vingine visivyo vya pombe, kama vya kuchochea nguvu mwilini na vinywaji vya malt na soda.

"Awamu ya tatu, ilianza Novemba Mosi, mwaka 2020 ambayo ilijumuisha kusajili stempu za elektroniki kwenye juisi za matunda (pamoja na mchuzi wa zabibu), juisi za mboga na maji ya kunywa ya chupa," alisema.

Minja alisema takwimu zinaonyesha makusanyo ya kodi ya ushuru wa bidhaa yameongezeka kwa asilimia 60 ikiwa miaka mitatu kabla ya kutolewa kwa ETS kwenye bia, mvinyo na pombe na italinganishwa na kipindi kama hicho baada ya kutolewa.

Alisema walikusanya Sh. bilioni 297.2 kama kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye bia, mvinyo na pombe katika kipindi cha miaka mitatu kabla ya Januari 15, mwaka 2019, lakini kutoka wakati huo hadi mwezi Juni mwaka huu, kiasi hicho kiliongezeka hadi Sh. bilioni 476.7.

Alisema ushuru wa bidhaa na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye bia zimepanda kwa asilimia 15 wakati ile ya vinywaji baridi imepanda kwa asilimia 29 huku kodi ya ushuru wa bidhaa na VAT kwenye maji ya chupa imepanda kwa karibu asilimia 156.

"ETS inaiwezesha serikali kutumia teknolojia ya kisasa kupata takwimu za uzalishaji kwa wakati unaofaa kutoka kwa wazalishaji. Kwa njia hii haiwezeshi tu serikali kukusanya kiwango sahihi cha kodi ya bidhaa pia inazuia kuingia kwa bidhaa bandia sokoni," alisema.

## Shule ya Jokate yasaidiwa vifaa TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Vodacom Tanzania Foundation jana ilikabidhi mchango wa vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Jokate Mwegelo iliyoko wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani.

Msaada uliokabidhiwa ni mwendelezo wa mkakati wa kampuni hiyo ya simu katika kuwaongezea wasichana uwezo katika fani za Hisabati, Sayansi na TEHAMA.

Vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. 37,856,170 vimekabidhiwa na Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, katika hafla iliyofanyika viwanja vya shule hiyo. Vifaa hivyo vinategemewa kuwanufaisha wanafunzi 150 wanaosoma katika shule hiyo.

Mworia alisema: "Tunafanya hivi kwa lengo la kujenga jamii jumuishi na isiyotenga baadhi ya watu wake kwa sababu za kijinsia, uwezo, kiuchumi wala ulemavu, tukiamini kwamba kila mmoja wetu ana nafasi yake katika jamii, ana mchango wake kwa maendeleo ya jamii zetu na taifa na pia kila mmoja wetu anastahili kunufaika na matunda ya maendeleo yanayopatikana nchini mwetu."

Vifaa vilivyokabidhiwa ni kompyuta 15, viti 15, meza 15, TV moja ya inchi 65 na kipanga njia (Router) na kwamba mchango huu unalenga kusaidia walimu kutoa mafunzo bora ya TEHAMA na kwa wanafunzi kujenga tabia njema za kujisomea pamoja na kujiamini kutokana na stadi za kiteknolojia watakazozipata.

Akipokea msaada huo, kwa niaba ya shule, Mkuu wa hiyo, Nixon Simon, aliishukuru Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, huku akiongeza kwamba:

"Wilaya ya Kisarawe imekuwa ikijitahidi kupambana na changamoto mbalimbali zinazosababisha wanafunzi waende nje ya maeneo yao kutafuta elimu kama hii ya TEHAMA, kufuatia mchango huu, tunaamini kuwa tutakuwa na uwezo wa kutoa huduma hii muhimu kwa walengwa wetu hapa hapa Kisarawe."

HABARI KIMATAIFA

## Duterte ampasia mwanawe kijiti urais

**Manila,** UFILIPINO

RAIS wa Ufilipino, Rodrigo Duterte, amesema binti yake Sara, atawania nafasi ya urais mwakani, huku binafsi akitangaza kuachana na siasa.

Sara Duterte-Carpio, binti ambaye atawania urais katika uchaguzi wa 2022 amekuwa msaidizi wa muda mrefu wa baba yake, hivi sasa ni Meya wa Davao, jiji la tatu kwa ukubwa Ufilipino atawania urais, licha ya awali kusema hatogombea nafasi yoyote ya kitaifa mwakani.

Katika mahojiano ya Rais Duterte na kituo cha televisheni cha ABS-CBN News, alibainisha wazi nia yake ya kuachana na siasa.

Rais Duterte alisema anajiuzulu siasa na hatagombea katika uchaguzi mkuu wa mwaka ujao.

Duterte mwenye umri wa miaka 76, mwezi uliopita alisema kuwa atagombea kiti cha makamu wa rais mwaka 2022. Katiba ya nchi hiyo inawaruhusu marais kuhudumu muhula mmoja wa miaka sita pekee.



Rais wa Ufilipino Rodrigo Duterte akiwa na binti yake Sara Duterte-Carpio wakihudhuria kwenye hafla mojawapo jijini Tokyo, Japan. Binti huyo anawania urais mwakani. **PICHA: MAKTABA**

Duterte, mtu mwenye utata na nguvu, aliingia mamlakani mwaka 2016 na aliahidi kupunguza uhalifu na kutatua mzozo wa dawa ya kulevya nchini humo.

Binti yake, Sara, ametoa ujumbe mseto juu ya kugombea nafasi ya urais.

Mwezi uliopita, Sara alisema kuwa hatajiunga na kinyang'anyiro cha kuwania urais kwa sababu yeye na baba yake wamekubaliana kuwa ni mmoja kati yao tu atakayegombea katika uchaguzi ujao utakaofanyika mwezi Mei, mwakani.

Hata hivyo, aliongoza katika kura zote za maoni zilizofanyika mwaka huu.

Tangazao la ghafla la kujiuzulu kwa Rais Duterte alilitoa mjini Manila katika eneo ambalo alikuwa anatarajiwa kujisajili kama mgombea. **REUTERS**

## DRC kushirikiana na WHO kuchunguza kashfa ya ngono

**Kinshasa,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi (pichani), amesema anataka ushirikiano wa kweli na Shirika la Afya Duniani (WHO), kuchunguza tuhuma za ubakaji na unyanyasaji wa kingono.



Amesema tuhuma hizo zinawakabili watumishi wa shirika hilo waliopelekwa kupambana na mlipuko wa ebola, DRC.

Msemaji wa serikali, Patrick Muyaya, alikiambia kituo cha televisheni cha taifa, mwishoni mwa wiki, kwamba Rais Tshisekedi alitoa wito huo wa kutaka ushirikiano wa dhati kati ya taasisi na vyombo vya serikali na mashirika ya kimataifa yaliyopewa jukumu la kufuatilia kashfa hiyo.

Wito huo aliutoa baada ya ripoti iliyotolewa ikibaini kasoro kubwa katika mfumo wa kazi na uzembe wa watu miongoni mwa wafanyakazi wa WHO, baada ya wanawake kadhaa kuwaambia wapelelezi kwamba, waliambiwa wafanye vitendo vya ngono ili kupewa kazi au waliathiriwa wa ubakaji.

Ripoti hiyo ilizingatia tuhuma dhidi ya wafanyakazi wa Congo na wa kimataifa waliofanya kazi nchini humo, kupambana na mlipuko wa ebola kuanzia 2018 hadi 2020.

"Rais Tshisekedi ameeleza kusikitishwa kwake na kulaani vitendo hivyo viovu na wakati huo huo kusifu ushujaa wa WHO, kwa kulaani hadharani uhalifu uliotendwa na wafanyakazi wake," alisema msemaji wa serikali. **VOA**


AccessBank
TANZANIA • ACCESS GROUP

ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE |
|---|---|
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | **TZS** |
| AGRO LOANS TZS 500,000 to 50,000,000 | from 49.2% to 68.4% with graduation for good repeat clients and with good account turnover. |
| **Loan Processing Fee** | **TZS** |
| AGRO LOANS TZS 500,000 to 50,000,000 | 3.70% Inclusive of excise duty and VAT |
| **Application Fee** | **TZS** |
| AGRO LOANS TZS 500,000 to 50,000,000 | 20,000.00 |
| **Insurance Fee** | **TZS** |
| AGRO LOANS TZS 500,000 to 50,000,000 | 2.0% |

216489801

# NMB BONGE LA MPANGO SASA YAREJEA NA ZAWADI MIL. 246/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imerejea na Promosheni ya Bonge la Mpango awamu ya pili ambapo kwa sasa imewatengea washindi zawadi zenye thamani ya shilingi milioni 246 zitakazoshindaniwa kwa miezi mitatu.

**Akizungumza wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara NMB, Filbert Mponzi, alisema lengo ni kurejesha sehemu ya faida waliyoipata kutoka kwa wateja wao, lakini zaidi ni kujenga utamaduni wa Watanzania kuweka akiba benki.**

Mponzi alifafanua kuwa kampeni hiyo itawawezesha wateja kushinda fedha taslimu na pikipiki za miguu mitatu maarufu kwa jina la Toyo ikiwa ni mwendelezo wa kampeni iliyopita ambapo mshindi alijishindia gari jipya aina ya Toyota Fortuner.

"Kama mnakumbuka, awamu ya kwanza ya Bonge la Mpango mwaka huu tulipata mshindi mmoja wa Toyota Fortuner, watatu wakajinyakulia TATA Mid- Sized Pick-up almaarufu kama Kirikuu, 24 walioshinda Lifan 3- wheeler (Pikipiki za miguu mitatu) na washindi 120 waliwekewa kiwango cha Sh. 100,000 hadi 500,000/- kwenye akaunti zao.

"Kikubwa zaidi, katika kampeni hii, zaidi ya shilingi milioni 246 zitatumika kutoa zawadi kwa washindi, huu ukiwa ni mkakati wetu kama benki kwa mwaka 2021 ambapo tunakusudia kuendelea kuifanya NMB kuwa chaguo namba moja kwa usalama wa fedha za wateja, suluhisho za kifedha na kwa faida," alisema Mponzi.

Aidha, alisema wateja wote wa NMB wa sasa na wale watakaofungua akaunti mpya wana nafasi ya kushinda zawadi ya Toyo 50 kila moja ikiwa na gharama ya Sh. milioni 4.4. Lakini pia washindi 120 watajishindia kila mmoja Sh. 100,000 jumla ikiwa fedha taslimu Sh. milioni 12.

Alisema wateja wanaofungua akaunti za NMB kwa mara ya kwanza, wakaweka kiasi cha Sh. 100,000, au kuhamisha Sh. 100,000 kutoka kwenye benki zingine na hata mitandao mingine ya simu watajishindia zawadi mbalimbali kutoka NMB kila wiki na kila mwezi.

Kwa wale ambao watafungua akaunti ya NMB au wateja wenye akaunti ya NMB na watakaoweka kiwango cha chini cha Sh. 100,000 kwa muda usiopungua mwezi mmoja, watajiongezea nafasi ya kuingia kwenye droo ya fainali itakayochezeshwa mwishoni mwa Desemba ambapo Toyo 14 zenye thamani ya Sh. milioni 62 zitatolewa.

Mponzi alibainisha: "Katika kipindi hiki cha mavuno kwa wateja wetu, tunatoa fursa pia kwa Watanzania wote kufungua akaunti kwetu ili kuingia kwenye orodha ya washindi na pia kupata fursa ya kutunza akiba kwa njia salama zaidi na NMB. Kwa hili, NMB inasema hii ndio Bonge la Mpango awamu ya pili kwa mwaka huu."

Itakumbukwa hivi karibuni Benki ya NMB ilipata tuzo sita za ubora ikionyesha ni benki inayoongoza kwa utoaji huduma bora kwa wateja wake nchini, hivyo ubunifu wa kipekee katika kuhamasisha Watanzania kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba ni miongoni mwa sifa za kipekee za benki hiyo.



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akiwa amepanda moja kati ya pikipiki za matairi matatu (Toyo) zitakazoshindaniwa katika Promosheni ya Bonge la Mpango awamu ya pili baada ya kuzinduliwa rasmi Dar es Salaam, ikiwa na lengo la kuhamasisha nidhamu ya kuweka akiba kwa wateja. Wapili kushoto ni Mhazini Mkuu wa NMB, Aziz Chacha, kuanzia kulia ni Ofisa Mkuu Raslimali Watu, Emmanuel Akonaay, Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi, Aikansia Muro, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Benedicto Baragomwa na Daniel Mbotto, Ofisa Mkuu wa Mikopo (katikati). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Baba Levo apewa shavu Active Media

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya (Bongo Fleva), Clayton Chipando, maarufu kama Baba Levo, amechaguliwa kuwa msemaji wa Active Media ambayo iko chini ya Kampuni ya The Active, inayojishughulisha na masuala ya matangazo na masoko ya bidhaa na huduma mbalimbali nchini.

'Active Media' ni jukwaa kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za vikao, matukio, masoko na matangazo mbalimbali ya bidhaa za makampuni yanayofanya kazi na Kampuni ya The Active kupitia mtandao wa YouTube.

Baadhi ya makampuni hayo ni pamoja na kampuni zinayotengeneza VIMTO, Unilever kupitia bidhaa zake za OMO na VASELINE pamoja na kampuni ya mawasiliano ya Zantel.

Akizungumza na vyombo vya habari wakati wa kumtambulisha rasmi msanii huyo, Meneja Mkuu wa The Active, Caroline Muia alisema Baba Levo anakuwa msemaji kwenye matukio yote yatakayoratibiwa na kampuni hiyo ili kuleta utofauti kwenye soko.

"Baba Levo atakuwa anafanya matangazo ya awali (Teasers) kuhusu matukio mbalimbali kupitia mtandao wa YouTube wa Active Media kabla, wakati na baada ya tukio husika inapohitajika. Pia, atakuwa mshereheshaji katika baadhi ya matukio hayo," alisema.

Muia alieleza kuwa Kampuni ya The Active imekuwa ikifanya shughuli za matangazo na masoko kwa njia ya kawaida (on ground marketing), lakini imeona ni vema kuongeza njia ya kidijitali ili kupanua wigo wa shughuli zake na kufikia wateja wengi zaidi.

"Wote mtakubaliana na mimi kuwa kwa sasa Tanzania inapitia mageuzi makubwa ya Kidigitali, yanayoakisiwa na idadi kubwa ya watu waliounganishwa na huduma za mawasiliano na intaneti. Wananchi wengi ambao pia ni wateja wetu, wapo kwenye mitandao mbalimbali," alisema.

# *Kim Poulsen ruksa kumtumia Kibu Taifa Stars*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa, 'Taifa Stars', Kim Poulsen, sasa ana uhuru wa kumchagua straika wa Simba Kibu Denis, baada ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutangaza kumpa uraia wa Tanzania.

Taarifa iliyotolewa na wizara hiyo jana kwenye mtandao wake wa kijamii ilisema: "Kufuatia Mamlaka aliyopewa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura ya 357 (Rejeo la 2002), baada ya kupokea ombi lililoletwa kwake na TFF, amempa uraia wa Tanzania Mchezaji wa Mpira wa Miguu, Kibu Denis Prosper, Sept. 30, 2021".

Baada ya tamko hilo, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo, aliliambia Nipashe kuwa kwa sasa wanaliacha suala hilo kwa kocha mwenyewe, kwani ni yeye ndiye aliyesema kuwa anamhitaji, na ndiye anayeweza kumuita.

"Tumelisikia hilo, lakini mpaka sasa kocha hajamuita kwenye kikosi, lakini tuvute subira kwa sababu Kocha Mkuu wa Taifa Stars ndiye mwenye mamlaka ya kumuita mchezaji kwenye kikosi cha taifa. Kwa sasa ameishaita kikosi chake, lakini kama anamhitaji atamuita kwa sababu alishasema alikuwa kwenye mipango yake. Haitokuwa mara ya kwanza kwa kocha kufanya hivyo, makocha wameshawahi kuwaita wachezaji, halafu baadaye wakaita mchezaji mmoja au wawili kuongezea nguvu," alisema Ndimbo.

Hivi karibuni, wakati akitangaza kikosi kilichoingia kambini jana, Poulsen alisema kuwa alimhitaji Kibu kwa kuwa yupo kwenye mipango yake, lakini alikuwa na changamoto ya suala la uraia, hivyo kushindwa kumjumisha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NUNEZ ANUKIA MAN CITY

MANCHESTER City wanaamini watawazima wapinzani wao Liverpool, Manchester United, Chelsea na Bayern Munich kwenye mbio za kuwania kumsajili straika wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22. ***(Star)***

### PHILLIPS KUONGEZA MKATABA

KIUNGO wa Leeds United na England, Kalvin Phillips, anatarajia kusaini mkataba mpya pale Elland Road. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, bado ana mkataba wa miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa. ***(Athletic)***

### CAVANI KUTUA REAL MADRID

STRAIKA wa Manchester United na Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, anaweza kujiunga na Real Madrid Januari, baada ya kushindwa kupata namba pale Old Trafford baada ya ujio wa Cristiano Ronaldo. ***(Mundo Deportivo)***

### UTD KUAMUA KWA POGBA

MANCHESTER United inataka kufanya mamuzi ya mwisho kuhusu majaliwa ya kiungo wake, Mfaransa Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, wakati wa kipindi cha Krismasi. ***(Sun)***

### GNABRY NA MKATABA MPYA

BAYERN Munich wanakaribia kumpa mkataba mpya mshambuliaji Serge Gnabry mwenye umri wa miaka 26. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

### HALAAND NJIA NYEUPE PSG

KLABU ya Paris St-Germain imeripotiwa ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Norway na Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### NANDEZ ATEGWA SPURS

KIUNGO wa Cagliari, Nahitan Nandez mwenye umri wa miaka 25, anapanga kuondoka klabuni hapo, kwa mujibu wa wakala wake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay amekuwa akiwaniwa na Tottenham Hotspur, Leeds pamoja na Napoli. ***(Calcio Napoli 24)***

### BRUCE KUBAKIA NEWCASTLE

STEVE Bruce atabaki kama kocha wa Newcastle wakati mmliki wa klabu hiyo, Mike Ashley akiendelea kutafuta mnunuzi wa timu hiyo. ***(Sun)***

### BENZEMA AMSUBIRI MBAPPE

STRAIKA wa Ufaransa, Karim Benzema mwenye umri wa miaka 33, ana uhakika kwamba mchezaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 22, atajiunga na Real Madrid siku moja. ***(L'Equipe via Sun)***

### POGBA APELEKWA MADRID

REAL Madrid imepewa ofa ya kumsajili Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, kipindi cha majira ya joto kijacho na wakala wake, Mino Raiola. ***(Express)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SUAREZ AFUNGUKA SAKATA KUMZOMEA KOEMAN BARCA

**Nilishajua kama nitafunga nitatakiwa kuomba radhi, lakini ishara ya kuongea na simu haikuwa...**

**MADRID,** Hispania

LUIS Suarez amesisitiza staili ya kushangilia kwake kwa kuonyesha ishara ya kuongea na simu wakati Atletico Madrid wakiibuka na ushindi dhidi ya Barcelona haikuwa na maana ya kumzomea kocha wake wa zamani, Ronald Koeman.

**Suarez alifunga bao wakati mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, Atletico wakiongeza presha kwa Koeman pale Barca, walipoibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano, juzi Jumamosi.**

Suarez raia wa Uruguay aliunganisha vizuri pasi ya Thomas Lemar na kufunga bao dakika ya 44 wakati shuti lake liliposhindwa kuokolewa na golikipa Marc-Andre ter Stegen, likiwa bao lake la nne msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, hakusherehekea haraka baada ya kufunga bao hilo, akionekana kuomba msamaha kwa mashabiki wa timu yake hiyo ya zamani, Barca ambayo aliifungia mabao 198 katika mechi 283 pamoja na kutoa pasi za mwisho 97.

Hata hivyo, alionekana akionyesha ishara ya kuongea na simu na kutoa tafsiri kwamba alikuwa anamzodoa kocha wake wa zamani Koeman, ambaye alimjulisha kuwa hayupo kwenye mipango yake baada ya kuchukuwa mikoba ya ukocha pale Camp Nou, Agosti mwaka 2020.

Lakini Suarez amesema ishara hiyo aliifanya kwa ajili ya familia yake na si vinginevyo.

"Tayari nilishajua kwamba, kama nitafunga nitatakiwa kuomba radhi," alisema Suarez akiwaambia waandishi wa habari.

"(Ishara ya kuongea na simu) ilikuwa kwa watu ambao wanajua nina namba zao na maalumu kwa ajili ya familia yangu.

"Haikuwa kwa ajili ya Koeman; nilikuwa nafanya utani na watoto wangu kwamba nitakuwa nafanya hivyo."

Ushindi huo wa 2-0 umeifanya Atletico kushindi katika mechi ya tatu mfululizo bila kuruhusu bao dhidi ya Barca kwa mara ya kwanza kwenye historia ya LaLiga.







# SOLSKJAER HAJUTII RONALD KUSUGUA BENCHI UNITED



**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema hajutii kumwanzishia benchi Cristiano Ronaldo wakati Manchester United wakilazimisha sare ya bao 1-1 na Everton, Jumamosi.

Kocha huyo wa 'Mashetani Wekundu' hao alifanya mabadiliko matano kutoka kwenye kiosi kilichocheza na Villarreal kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano wakipata ushindi kwa bao la dakika ya mwisho la Ronaldo.

Ronaldo alianzia benchi na Anthony Martial alianza kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu England tangu Agosti, na alifunga kwa mara ya kwanza tangu Februari na kuifanya United kuwa mbele.

Martial alitolewa na ndani ya dakika 10 baada ya Solskjaer kuwaingiza Ronaldo na Jadon Sancho, Everton wakasawazisha kupitia Andros Townsend.

United walionekana kubanwa kila sehemu na walifungwa bao la pili lilipachikwa wavuni na Yerry Mina, lakini lilikataliwa na VAR.

Man sasa wameshinda mechi mbili kati ya sita zilizopita kwenye mashindano yote.



# *Arteta: Arsenal bado inahitaji kujiimarisha*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekubali kuwa Arsenal haikustahili kushinda baada ya kutoka suluhu na Brighton and Hove Albion, kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

'Washikabunduki' hao walikuwa wakitarajia kushinda mchezo wao wa nne, lakini wakajikuta wakibanwa na 'Seagulls' hao na sasa timu zote mbili zimefikisha mechi tano bila kupoteza.

Mpira wa kichwa wa Pierre-Emerick Aubameyang uligonga mwamba na Emile Smith-Rowe akikaribia kufunga kipindi cha pili.

Na Kocha Mkuu, Arteta alisema baada ya mchezo huo kuwa, Washikabunduki hao wanatakiwa kujiimarisha zaidi baada ya kushindwa kupata ushindi pale kwenye dimba la Amex.

"Ninachofikiria ni namna tulivyocheza," alisema Arteta akiiambia BBC Sport baada ya mchezo huo.


"Hatukufanya maamuzi sahihi, kila wakati tulishindwa kuendana na presha ya mchezo na hatukushambulia kwa kasi.

"Nafasi ya Aubameyang pengine ndio ilikuwa ya wazi zaidi ya kuweza kufunga katika kipindi cha kwanza, na hatukuwa na bahati ya kufunga.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY

# IQUE AKIRI ARCA KUNA ATATIZO AKUBWA




**RCELONA,** Hispania

GERARD Pique amekubali Barcelona haikuwa bora wakati wakichezea kichapo kutoka kwa Atletico Madrid na amesema hata kama wangecheza kwa saa tatu wasgeweza kufunga bao.

Miamba hao wa Catalunya walikumbana na pigo cha pili mfululizo kwenye mashindano te na mchezo wao wa kwanza kwenye LaLiga ngu Mei - wakati walipofungwa mabao 2-0, Jumosi.

Barca walipiga mashuti mawili tu ya kulenga o katika dakika zote 90 kwenye mchezo huo opigwa Uwanja wa Wanda Metropolitano.

Memphis Depay, ambaye amekuwa na mashuti engi ya kulenga bao kwenye LaLiga (13, sawa na rim Benzema wa Real Madrdi, hakufurukuta pisa kwenye mchezo huo.

Atletico walikuwa kwenye kiwango bora, wakinga mabao mawili katika mashuti sita yaliyolenbao, Luis Suarez alitengeneza bao la kwanza lilfungwa na Thomas Lemar kabla yeye kufunga pili.

Barca sasa imeruhusu mabao matano bila wao funga katika mechi mbili zilizopita, na Pique, baye alikuwa sehemu ya kikosi wakati wakingwa na Benfica kwenye Ligi ya Mabingwa aya katikati ya wiki, amesema kikosi chao kinaaji kufanya kazi ya ziada.




wa Bonasi ya Jackpot, Yusuph Jaivi kutoka kionyesha mfano wa hundi ya Sh. 15,610,066 a kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

# *Washindi Jackpot Bonus SportPesa waongezeka*

**Na Mwandishi Wetu**

KWA wiki nyingine tena Kampuni ya Michezo na Burudani ya SportPesa, imetoa bonus kwa washindi wake waliobashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot yao ya kila wiki.

Mpaka sasa Jackpot imefika shilingi 537,737,060 kutokana na kuongezeka kila wiki endapo mshindi hakupatikana.

Wiki iliyopita idadi ya washindi waliopatia kwa usahihi mechi 10 walikuwa 660 na kila mmoja aliondoka na Sh. 70,013 huku , waliopatia kwa usahihi mechi 11 wakiwa 83 na kila mmoja akiondoka na kiasi cha shilingi 487,141 na wale waliobashiri kwa usahihi mechi 12 walishinda 15,610,066 kila mmoja.

SportPesa huhakikisha washindi wote wanakabidhiwa pesa zao mara tu mechi zote zimalizikapo na endapo michezo isiyozidi mitatu ikiahirishwa basi droo ya wazi huchezeshwa ili kupata matokeo na ikiwa mechi zaidi ya tatu zimeahirishwa basi fedha zote hurudishwa kwenye akaunti ya mteja.

Waliojishindia Sh. 15,610,066 walikuwa nane kutoka sehemu mbalimbali nchini ambao ni Richard Magele kutoka Geita, wakati kutoka Dar es Salaam ni Sengo Lubasha, Mohammedwaseem Gjartem na Ramadhan Chiwango, wengine wakiwa ni Enock Ernest (Musoma), Jabil Mwanjoa na Yusuph Jaivi (Lindi) na Amin Ally kutoka Kagera mjini.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 04 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1270 | Leixoes SC U23 vs Rio Ave U23 | 2.50 | 3.30 | 2.80 |
| 14:00 | 5352 | Swansea U23 vs Ipswich U23 | 2.03 | 3.44 | 3.20 |
| 15:00 | 2484 | Sheffield Wednesday U23 vs Barnsley U23 | 3.78 | 3.88 | 1.75 |
| 16:00 | 2661 | Charlton U23 vs Colchester U23 | 1.98 | 3.98 | 2.96 |
| 16:00 | 2999 | PFC Minyor Pernik vs Strumska Slava | 1.47 | 3.96 | 6.18 |
| 16:00 | 4104 | Cruzeiro MG U20 vs Santos SP U20 | 1.63 | 4.30 | 4.60 |
| 16:00 | 5467 | AZ Picerno vs Catania | 3.17 | 3.07 | 2.33 |
| 17:00 | 1677 | CF Belenenses U23 vs SC Farense U23 | 1.69 | 3.72 | 4.25 |
| 17:00 | 4878 | Cobresal vs Audax Italiano | 1.76 | 3.38 | 4.35 |
| 19:00 | 4026 | GKS Jastrzebie Zdroj vs Arka Gdynia | 4.66 | 3.84 | 1.61 |
| 19:00 | 4167 | Notodden vs Rosenborg BK 2 | 1.34 | 5.03 | 6.58 |
| 20:00 | 2610 | Skeid Fotball vs Odds BK 2 | 1.44 | 4.53 | 5.60 |
| 20:00 | 3281 | Vasalunds IF vs IFK Varnamo | 4.21 | 3.86 | 1.77 |
| 20:00 | 3895 | Magdeburg vs Turkgucu Ataspor Munchen | 1.77 | 3.59 | 4.23 |
| 20:00 | 4784 | Eidsvold Turn vs Valerenga IF 2 | 1.65 | 4.18 | 3.99 |
| 20:00 | 5280 | IK Brage vs Osters IF | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 20:00 | 5440 | Esbjerg vs HB Koge | 1.91 | 3.44 | 3.58 |
| 20:00 | 5703 | Santa Lucia Cotzumalguapa FC vs Deportivo Malacateco | 1.70 | 3.39 | 4.75 |
| 20:30 | 5340 | Clinceni vs Botosani | 4.13 | 3.39 | 1.84 |
| 21:00 | 1576 | Leandro N Alem vs Excursionistas | 2.81 | 2.86 | 2.57 |
| 21:00 | 1593 | Argentino Merlo vs Central Cordoba | 2.29 | 2.85 | 3.24 |
| 21:00 | 1791 | West Bromwich U23 vs Sunderland U23 | 1.81 | 3.88 | 3.49 |
| 21:00 | 2152 | Nyiregyhaza vs Bgsz Siofok | 1.99 | 3.35 | 3.40 |
| 21:00 | 2369 | CA Atlanta vs Agropecuario | 2.57 | 2.72 | 2.96 |
| 21:00 | 2920 | Defensores Belgrano vs Santamarina | 2.15 | 2.76 | 3.73 |
| 21:00 | 4489 | General Lamadrid vs Ferrocarril Midland | 2.07 | 2.91 | 3.73 |
| 21:00 | 4710 | Corinthians SP U20 vs Atletico PR U20 | 2.48 | 3.85 | 2.50 |
| 21:00 | 4994 | Reading U23 vs Birmingham U23 | 2.66 | 3.57 | 2.28 |
| 21:45 | 3065 | Crusaders Belfast vs Coleraine FC | 2.56 | 3.53 | 2.37 |
| 22:00 | 1308 | Puerto Montt vs Rangers | 2.29 | 2.90 | 3.19 |
| 22:00 | 2216 | Girona vs Almeria | 2.62 | 3.07 | 2.72 |
| 22:00 | 3353 | Rubio NU vs Fulgencio Yegros | 2.11 | 3.00 | 3.48 |
| 22:00 | 3731 | Juve Stabia vs Palermo | 2.39 | 3.07 | 3.07 |
| 22:00 | 5479 | Annecy FC vs Villefranche Sur Saone | 2.29 | 3.08 | 3.08 |
| 22:15 | 4663 | CD Trofense vs Nacional Madeira | 2.78 | 3.17 | 2.44 |
| 22:15 | 4810 | Vasco DA Gama RJ U20 vs Palmeiras SP U20 | 2.39 | 3.48 | 2.57 |
| 23:00 | 2769 | Llaneros FC vs Leones FC | 2.14 | 3.07 | 3.31 |
| 23:10 | 4212 | San Martin Tucuman vs Gimnasia Mendoza | 2.05 | 2.99 | 3.67 |

### JUMANNE - 05 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 2876 | Defensa Justicia vs Talleres | 2.90 | 2.85 | 2.51 |
| 00:30 | 2634 | Melipilla vs Santiago Wanderers | 2.62 | 3.15 | 2.52 |
| 01:00 | 3393 | Necaxa W vs Queretaro W | 3.23 | 3.48 | 2.01 |
| 01:00 | 5285 | Sp. San Lorenzo vs Tacuary Asuncion | 2.90 | 2.90 | 2.47 |
| 02:00 | 3637 | Remo PA vs Coritiba | 2.99 | 2.94 | 2.37 |
| 02:15 | 5294 | Colon Santa Fe vs Banfield | 2.28 | 3.00 | 3.10 |
| 03:00 | 1268 | Huachipato vs Curico Unido | 2.12 | 3.24 | 3.19 |
| 03:00 | 1554 | Monterrey W vs Leon W | 1.12 | 7.33 | 15.43 |
| 03:00 | 4190 | America W vs Cruz Azul W | 1.38 | 4.53 | 6.74 |
| 03:00 | 5146 | Delfin SC vs Manta | 1.77 | 3.39 | 4.26 |
| 03:10 | 4500 | Almirante Brown vs Estudiantes Rio Cuarto | 1.94 | 2.90 | 4.25 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Oktoba 4, 2021
Nipashe



Arteta: Arsenal bado inahitaji kujiimarisha UKURASA 22

# Nabi aipeleka Yanga SC kucheza za kimataifa

## ●●● Kujichimbia Arusha kabla ya kurejea kupiga mechi moja kwa Mkapa kisha...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya kupata pointi sita kwenye mechi mbili za mwanzo za Ligi Kuu Tanzania Bara, timu ya Yanga inatarajia kucheza mechi mbili za kimataifa, moja ikiwa nje ya nchi, imeelezwa.

**Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, awaambia waandishi wetu kuwa kutokana na mapumziko ya muda mrefu baada ya mechi mbili za Ligi Kuu, Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, ameomba mechi mbili za kirafiki ili kuwaweka wachezaji wake kwenye utimamu mzuri kimwili na kuendelea kuwa fiti hata baada ya ligi kurejea.**

"Kuna muda mrefu ligi itasimama. Kuna mapumziko ya mechi za kimataifa za timu za taifa, tutacheza tena dhidi ya KMC FC Oktoba 19, kwa hiyo kipindi hiki kama uongozi tumepokea mapendekezo ya mwalimu Nabi, Tunapanga kutafuta mechi mbili za kimataifa na timu za nje ya nchi. Moja tutacheza hapa Dar es Salaam na nyingine tunaweza kwenda kucheza nje ya nchi," alisema Bumbuli.

Yanga imecheza mechi mbili za Ligi Kuu, zote ikishinda bao 1-0, Jumatano iliyopita ikiichakaza Kagera Sugar, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba na Jumamosi ikashinda tena dhidi ya Geita Gold kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumzia mechi iliyopita dhidi ya Geita Gold FC, pamoja na kuwapongeza wachezaji wake kwa ushindi, Nabi alisema bado anahitaji kufanyia kazi safu ya ushambuliaji na kuhakikisha wachezaji wote wanakuwa fiti kucheza dakika 90 za mchezo kwa ubora.

"Mechi ilikuwa nzuri kwa pande zote mbili, kwetu tumetengeneza nafasi nyingi, washambuliaji wangu wangekuwa makini tulitakiwa kufunga mabao mengi, lakini pia tunacheza vizuri kipindi cha kwanza na kipindi cha pili tunakata pumzi.

"Kipindi hiki cha mapumziko ya timu za taifa, natarajia kuondoka na wachezaji waliobaki kwenda Arusha kwa ajili ya kufanyia kazi safu ya ushambuliaji pamoja na 'fitness' kwa wachezaji waweze kucheza kwa kiwango kizuri kwa dakika zote 90 za mchezo," alisema Nabi.

Alisema atakapokuwa Arusha atakuwa na muda mwingi wa kufanyia kazi mapungufu ya timu yake yaliyojitokeza katika michezo miwili waliyocheza ikiwamo dhidi ya Kagera Sugar na Geita Gold FC.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Geita Gold FC, Felix Minziro, alisema wamepokea matokeo hayo na ana imani tatizo kubwa liko kwenye safu yao ya ushambuliaji kutokuwa makini na kukosa utulivu.

"Tatizo letu kubwa ni kukosa utulivu na umakini hasa katika safu ya ushambuliaji, tungetulia na kutumia vizuri nafasi tulizotengeneza basi muda huu tungekuwa tunaongea mengine," alisema Minziro.

Ligi Kuu Tanzania Bara itasimama kwa wiki moja na ushehe kupisha mechi za kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, ambapo wachezaji wa klabu mbalimbali wamekwenda kuzitumikia timu zao za taifa.

RUKSA STARS...



Straika wa Simba, Denis Kibu, rasmi sasa ni raia wa Tanzania, hivyo anaruhusiwa kuichezea Taifa Stars na klabu yake baada ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kutangaza juzi. **HABARI UK. 20**

# Sakho, Kennedy wako fiti - Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imewatoa hofu wanachama na mashabiki wao kuhusu hali za wachezaji Pape Sakho na Kennedy Juma walioumia kwenye mechi ya Ligi Kuu Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, dhidi ya Dodoma Jiji FC, kuwa hali zao zinaendelea vizuri na hawakupata majeraha makubwa sana.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, mratibu wa timu hiyo, Abbas Ally, alisema wachezaji hao wanaendelea vema na hawakupata majeraha ambayo yangeweza kuwaweka nje kwa muda mrefu, hivyo wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi.

"Kama ulivyoona ni kwamba Kennedy na Sakho waliumia na ikabidi wakimbizwe hospitali, tunashukuru baada ya kufika huko ikaonekana ni majeraha ya kawaida. Wakatibiwa na wamepewa mapumziko ya siku mbili kabla ya kuanza tena mazoezi," alisema mratibu huyo.

Kuhusu Thedeo Lwanga, alisema mchezaji huyo alipata maumivu ya pale pale uwanjani, lakini hakulazimika kukimbizwa hospitali, badala yake alitibiwa pale pale, hivyo yeye hakuwa na tatizo.

"Tunawatoa hofu mashabiki wa Simba kuwa wachezaji hao wako fiti na wataanza mazoezi na wenzao," alisema.

Aidha, Abbas, alisema wachezaji 14 wa kikosi hicho waliosalia wataanza mazoezi leo kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, Oktoba 15, mwaka huu, Simba ikianzia ugenini.

"Baada ya mechi dhidi ya Dodoma Jiji, wachezaji wetu walipata mapumziko ya siku mbili na Jumatatu (leo), wataanza mazoezi kwa 14 waliobaki kwa sababu wengi wao wamekwenda kuzitumikia timu zao za taifa, wa nje ya nchi na wale wa Taifa Stars," alisema.

Mashabiki wengi wa Simba walikuwa na hofu kuhusu hatima ya wachezaji wao, hasa ikizingatia ina mchezo wa kimataifa hivi karibuni.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042